Nipashe
Jumatano Desemba 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581880
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
Nipashe digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US
epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Kariakoo yote sasa kufungwa kamera

• **Zabuni** yatangazwa kipindi ambacho kuna timu inachunguza usalama wa majengo, wahalifu kitanzini... *Endelea Ukurasa 2*



Wananchi wakiwa kwenye pilikapilika katika moja ya mitaa ya eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

UKURASA WA 2

**Waziri** abaini wimbi uvamizi maeneo ya huduma za kijamii



UKURASA WA 5

**Mawakili** watakiwa kwenda kortini na nyaraka za kuthibitisha walikokuwa

UKURASA WA 19



**Kisa** waasi M23, DRC yaiburuza Rwanda kortini

UKURASA 4



## TRA yapata mwarobaini wa pombe feki sokoni



## Nondo asimulia yaliyojiri alipotekwa

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YATAMBIA UZOEFU MECHI CAF UK.24

MAONI, UK.6



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, akikabidhi hati ya umiliki wa ardhi kwa mkazi wa Chamwino Ikulu, Kanali Christina Ilahuka kwenye maadhimisho ya Wiki ya Ardhi Kitaifa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kariakoo yote sasa kufungwa kamera

**Na Restuta James**

SASA ni rasmi serikali inakusudia kufunga kamera za ulinzi (CCTV), katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, ili kudhibiti uhalifu na kuwezesha biashara kufanyika kwa saa 24.

Mkurugenzi wa Jiji la Ilala, juzi alitoa taarifa ya kumtafuta mzabuni akayetekeleza kazi hiyo na jana ilikuwa ni siku ya kutembelea eneo kamera zitakapofungwa, kuanzia Polisi Msimbazi.

Katika taarifa hiyo, mkurugenzi huyo alisema kazi hiyo inaweza kufanywa na kampuni binafsi, taasisi au ubia.

"Tangazo la usambazaji na ufungaji wa kamera za CCTV Kariakoo awamu ya kwanza... kampuni za serikali, za ndani, za kigeni, kikundi maalumu, mtengenezaji wa ndani, ubia, mtengenezaji wa nje ya nchi, ushirikiano wa kampuni za ndani na nje, wanaitwa kushiriki," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Ilieleza kuwa fedha za kufunga kamera hizo zimetengwa na serikali katika bajeti yake ya mwaka huu wa fedha, 2024/2025.

"Serikali imetenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025. Inakusudiwa kuwa sehemu ya mapato ya mfuko itatumika kulipia malipo stahiki chini ya mkataba wa ufungaji wa kamera ya CCTV awamu ya kwanza katika eneo la Kariakoo," ilifafanua.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema Kariakoo itafungwa kamera na taa, ikiwa ni kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, kutaka biashara katika eneo hilo zifanyike kwa saa 24.

"Tunafunga kamera na taa kwa pamoja. Lengo ni kuimarisha ulinzi na pia kuwezesha biashara zifanyike kwa saa 24," alisema.

Akiwa katika ziara ya kikazi mwezi uliopita, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema serikali inakusudia kufunga kamera hizo katika maeneo mbalimbali ya jiji ili kuimarisha ulinzi.

Alisema kamera na taa zitafungwa kwenye maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu ikiwamo Kariakoo.

Serikali inakusudia kufunga taa na kamera za ulinzi, wakati ambao Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ameunda Kamati ya Wataalamu ya Uchunguzi wa majengo katika eneo la Kariakoo.

Kamati hiyo iliundwa baada ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa tatu katika eneo la Kariakoo na kusababisha vifo vya watu 31 na wengine 88, kujeruhiwa Novemba 16, mwaka huu.

Aliiagiza itekeleze majukumu yake kwa kufuata sheria, kanuni na maadili ya kazi, kwa kuchunguza uimara wa majengo yanayojengwa, kuchunguza endapo taratibu zinafuatwa wakati wa ujenzi, ikiwamo vibali, makandarasi wenye sifa na usimamizi wa mamlaka husika wakati wa ujenzi.

Waziri Mkuu alisema madhumuni mengine ya kuundwa kwa kamati hiyo ni pamoja na kuchunguza endapo uboreshaji majengo unaofanywa Kariakoo unazingatia sheria, kanuni na taratibu pamoja na kubainisha majengo yote yaliyo katika hatari ya kuanguka na kupendekeza hatua za kuchukua.

Aidha, zinafungwa wakati ukarabati wa soko la Kariakoo ukiwa umefikia asilimia 90 na kugharimu Sh. bilioni 28.

Akiwa mkoani Kagera, Agosti mwaka huu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, alisema serikali iko mbioni kufunga kamera za uchunguzi 6,500 kwa kuanzia na majiji makuu manne, ili kupunguza uharibifu na kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi.

Alisema kamera zitafungwa katika maeneo ya mikusanyiko ya watu kama vile maeneo ya masoko, viwandani na kwenye kampuni katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma.

Aidha, kamera hizo zitafungwa chini ya mradi wa Jeshi la Polisi wa majiji salama na kwamba bajeti ya utekelezaji imetengwa katika mwaka huu wa fedha 2024/25.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Waziri abaini wimbi la uvamizi maeneo ya huduma za kijamii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, amebaini kuwapo wimbi la maeneo ya huduma za kijamii yakiwamo shule na nyumba za ibada kubadilishwa matumizi kwa kujengwa maduka ya biashara na baa.

Pia amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, kuendelea kuwachukulia hatua watumishi na kampuni za upimaji ardhi zinazobainika kuzalisha migogoro ya ardhi kwa kupima na kuuza maeneo ya wananchi.

Akifungua Wiki ya Ardhi jana jijini hapa, Waziri Ndejembi alisema wataalamu wametoa vibali vya kubadili matumizi maeneo ya makazi, huduma za kijamii na ya wazi yaliyotengwa yamekuwa ya biashara kinyume cha utaratibu.

Aliagiza wataalamu kuhakikisha mitaa inabaki kama ilivyopangwa kama ni biashara, makazi au huduma za kijamii.

"Nawaomba sana tumieni taaluma zenu katika kuhakikisha tunapanga miji yetu vizuri. Kuna mitaa imepimwa hata zimamoto haiwezi kuingia. Kuna kaugonjwa kameingia kakubadili matumizi maeneo ya makazi, kesho unakuta kuna fremu za biashara, baa kwenye eneo la makazi ya watu na ukifuatilia unakuta mabadiliko ya matumizi yamefanyika.

"Kuna maeneo mengi tu yamebadilishwa. Hata hapa Dodoma naweza kuwabeba niwapeleke muone najua kwenye mipango tumetenga maeneo ya shule, ya ibada lakini unakuja baadaye unabadili matumizi, tufanye kazi kwa weledi," alisema.

Kuhusu upimaji wa viwanja unaofanywa na sekta binafsi, Ndejembi alisema kumekuwa na kampuni zinazopima zimeanza kuuza viwanja bila makubaliano na watu waliowapa kazi ya kupima na kwamba tayari serikali imeanza kuchukua hatua na tayari kampuni kati ya tatu au nne zimefutwa hatua na kutaka kasi hiyo iongezeke.

"Migogoro mingi inazalishwa na kampuni hizi za kupima ardhi mezani kwangu ninayo zaidi ya 20. Tuanze kuchukua hatua mara moja kwa kampuni ambazo zinatuzalishia migogoro.

"Kwa mfano kuna mwananchi mmoja ameomba shamba lake lipimwe amefuata taratibu zote na akaunganishwa na kampuni binafsi ya kupima lakini ikapima na kuanza kuuza viwanja yenyewe bila mwananchi mwenye eneo lake kujua viwanja vimeanza kuuzwa alishtuka watu waliouziwa wanafanya maendelezo, kampuni ilipoulizwa inaingilia huku na kutokea huku. Ni muhimu watendaji wetu kuhakikisha wananchi wanakuwa salama," alisema.

Aliwataka watumishi wa sekta hiyo kuwa na nidhamu kuzingatia weledi na kujiepusha kuwa sehemu ya migogoro.

Kuhusu matumizi ya mfumo wa kidigitali wa e-ardhi, waziri huyo alisema umeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya halmashauri katika mikoa mitano ya Arusha, Dodoma, Pwani, Tabora na Shinyanga na unalenga kuleta mageuzi katika sekta ya ardhi nchi.

"Mfumo umezingatia maeneo yote muhimu ya utoaji wa huduma, umefungamanishwa na mifumo mingine ya serikali ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa zingine muhimu na kuleta ufanisi katika sekta ya ardhi kwa wananchi," alisema.

Alibainisha kuwa mfumo utaharakisha utoaji huduma, kuimarisha uwazi na uadilifu, kupunguza gharama na muda, kusaidia kufikia malengo yaliyowekwa kwenye makusanyo, utoaji hatimiliki, upimaji na uthamini wa ardhi.

Alisema mfumo huo utasaidia wananchi wa mijini na vijijini kupatiwa huduma kwa usawa bila urasimu.

"Nimepata taarifa kuwapo kwa watumishi wachache wanaokwepa kutumia mfumo kutoa huduma zinazotarajiwa kwa visingizio mbalimbali na kwa maslahi yao binafsi, nakuagiza Katibu Mkuu kila mtumishi ambaye mfumo huu umeanza kutumika ahakikishe anautumia kikamilifu na uendelee kuchukua hatua dhidi ya wasiotaka kuutumia," alisema.

Ndejembi alikemea watumishi wanaofanya kazi kwa mazoea na kuharibu taswira ya sekta hiyo na kwamba hatawavumilia watakaobainika kuanzisha migogoro kwa maslahi yao binafsi.

"Tunataka kuondoa sura iliyopo kwenye jamii, unapotamka Wizara ya Ardhi kitu cha kwanza kinachokuja kichwani mwa mwananchi ni mgogoro, na hii migogoro mingi inasababishwa na wale ambao sio waadilifu, nataka tutoke kwenye dhana ya Wizara ya Migogoro iwe Wizara inayotatua changamoto za wananchi," alisema.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Anthony Sanga, alisema katika wiki hiyo ya ardhi wataalamu watajadili masuala mbalimbali ikiwamo utafiti uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhusu sekta ya ardhi.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# CCM wamwita Lissu Singida wachuane kuwania ubunge

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida kimekitaka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuondokana na fikra kwamba katiba mpya ndio itakiwezesha kupata ushindi katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

Katibu wa CCM Wilaya ya Ikungi, Joshua Mbwana, amesema chama hicho cha upinzani kitambue kuwa wanaopiga kura ni wananchi na si katiba ambayo imekuwa inapigiwa kelele na viongozi wakuu wa CHADEMA wakidai Katiba mpya.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushindi ambao chama hicho kimeupata wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu.

"Niwaambie katiba haipigi kura, kinachopiga kura ni watu, watu hawa waliomwelewa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutokana na miradi mingi aliyoleta, ndio hawa hawa watakaopiga kura Uchaguzi Mkuu mwaka 2025," alisema.

Mbwana alipoulizwa iwapo Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Lissu, akijitokeza kugombea ubunge mwakani katika wilaya hiyo, alisema CCM inamkaribisha kama ana nia hiyo.

Hata hivyo, alidai mwanasiasa huyo atapata aibu kwa kupata kura chache kama ilivyotokea katika kijiji cha Mahambe alikozaliwa; kijiji na vitongoji vyote vimechukuliwa na CCM wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

# Nondo asimulia yaliyojiri

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Ngome ya Vijana wa Chama cha ACT-Wazalendo, Abdul Nondo, amesimulia alivyotekwa na kuteswa huku akisisitiza watekaji walimtishia atauawa endapo atasimulia lolote lililojiri walipomteka.

Nondo anayedaiwa kutekwa Desemba Mosi mwaka huu kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli, wilayani Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam, alitoa kauli hiyo jana akiwa Hospitali ya Aga Khan, jijini jana.

"Watekaji walinichukua kwa nguvu, licha ya kelele na vuta nikuvute, sikusaidika na kulikuwa na bodaboda moja na watu wengine wakiangalia tukio lile likiendelea, lakini hawakunisaidia.

"Walinifunga kitambaa cheusi kwenye macho, kamba mikononi... walinisafirisha kwa mwendo huku nikipigwa na baadaye walinining`iniza mahali, miguu juu huku wakinipiga kwenye unyao, walinipiga mgongoni na mikononi.

"Nilitolewa na kubadilishwa gari lingine... wakanifungua pingu, wakanifunga kamba na kunining`iniza katika gari dogo kutoka 'hardtop' kisha kunisukumiza kwenye fukwe hizo, wakaondoka...

"Nilihisi upepo na mawimbi ya bahari, ndipo nikapata msaada kwenda ofisi za chama. Nilikuwa na hali mbaya, sikuweza kwenda nyumbani maana ninaishi mwenyewe, hivyo salama yangu ilikuwa ni kwenda ofisini na ndipo nilipoletwa hospitalini," alisema Nondo.

Alisema haikuwa rahisi kwake kusikiliza mazungumzo ya waliomteka kwa kuwa walikuwa wananong`ona."Walikuwa wananong`onezana wao tu kiasi kwamba huwezi kusikiliza na kipindi hicho wamenifunga kitambaa cheusi kwenye macho, na wamenifunga kamba mikono na wameirudisha nyuma mgongoni.

"Walikuwa wananikanyaga na mwingine akaweka chuma katikati ya miguu halafu akaning`iniza juu, akawa ananipiga kwenye nyayo za miguu, ananipiga kwenye 'joint', ananipiga mgongoni, ananipiga tu, ananiambia 'wewe si cha mdomo, endelea, sisi tunakuua leo'. Yaani hakuna stori ambayo inaweza kunifanya kujua kwamba hawa watu walikuwa wanataka nini kwangu," alidai.

Nondo alidai watekaji walimwambia kwamba kilichomponza mpaka akatekwa "ni kuongeaongea sana".

Alidai watekaji walimwambia amekuwa akionywa mara kadhaa, lakini aliendelea kuzungumza, hivyo huo ulikuwa mwisho wake.

Nondo alidai kuwa baada ya kumtupa ufukweni, walimwambia akitoka huko aende moja kwa moja nyumbani kwake na asisimulie lolote mahali popote.

"Wakaniambia... 'haya ukitoka hapa moja kwa moja nenda nyumbani, na nyumbani kwako tunapajua, tusisikie unaongea chochote, tusisikie sijui unakwenda kwenye vyombo vya habari, tusisikie unamwambia yeyote, tukikusikia unafanya hivyo, awamu ya pili sisi tunakuja... tukikuchukua kama tulivyokuchukua leo, tunakuua, tunaweza tukakuchukua sehemu yoyote na hiyo awamu tukija kukuchukua tunakuua," alidai Nondo.

Mwenyekiti huyo alidaiwa kutekwa kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kuteremka kwenye basi, akitokea mkoani Kigoma, alikokuwa anashiriki kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alidai alichukuliwa kwa nguvu na watu sita ambao walimfunga mikono na miguu pamoja na kumfunika uso na baadaye kumpiga sehemu mbalimbali za mwili wake.



Dereva wa bodaboda akiwa amebeba abiria aliyebeba baiskeli katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mbuyuni, Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mfumo kidijitali kukusanya taarifa waathirika wa wanyamapori wakali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mfumo wa kidijitali wa kukusanya na kuchakata taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu uwandani ili kumaliza tatizo la ucheleweshaji taarifa za wananchi wanaoathiriwa kwa ajili ya ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua semina ya siku mbili kwa maofisa wanyamapori wa wilaya nchini.

"Ili kutatua changamoto hiyo wizara imeandaa mfumo wa kidijitali utakaotumika kukusanya na kuchakata taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu uwandani (PAIS) ili kuharakisha utoaji wa taarifa na taratibu katika ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wakati," alisema.

Pia alisema hivi sasa kumekuwapo malalamiko mengi kuhusu waathirika wa wanyamapori wakali na waharibifu kucheleweshewa malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kutokana na taarifa kutofika kwa wakati wizarani.

"Hivi sasa wabunge wengi wanalalamika lakini pia wananchi wanalalamika kucheleweshewa malipo yao kutokana na taarifa za matukio hayo kuchelewa kufika wizarani, hivyo mfumo huu utakwenda kumaliza tatizo hilo," alisema.

Alisema pamoja na mchango wa sekta ya maliasili na utalii katika uchumi na ustawi wa nchi na jamii bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Alisema migongano hiyo inayosababishwa na uvamizi wa shughuli za kibinadamu karibu na maeneo ya hifadhi na kwenye shoroba za wanayamapori hususani shughuli za kilimo, ufugaji na makazi ya kudumu na hivyo kupelekea kuzibwa kwa shoroba.

Pia alisema changamoto nyingine ni kuongezeka kwa vitendo vya ujangili wa wanyama na migogoro ya mipaka ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka maeneo yaliyohifadhiwa.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto za uhifadhi nchini ikiwa ni pamoja na kuandaa sera, kanuni,mikakati,mipango na miongozo mbalimbali.

Mkurugenzi wa Wanyamapori, Dk. Alexander Lobora, alisema semina hiyo inajumuisha maofisa wanyamapori wa wilaya nchini.

Alisema lengo ni kubadilishana uzoefu pamoja na kuwapatia mafunzo kuhusu mfumo huo wa ukusanyaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu uwandani ili kuharakisha mchakato wa malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kinachotolewa na serikali.

"Matukio ya mgangano baina ya wanyamapori na binadamu yanachangia sana katika kuathiri uchumi wa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla kuanzia mwenzi Julai mwaka huu hadi sasa serikali imeshalipa Sh. bilioni 2.5 kwa watu walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu," alisema.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi kuhusu baadhi ya huduma za urekebishaji wa viungo zinazotolewa na Hospitali ya CCBRT, alipotembelea banda lao, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# TRA yapata mwarobaini pombe feki sokoni

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetengeneza stempu maalumu za kielektroniki (ETS) kwa ajili ya vinywaji vikali kudhibiti pombe feki sokoni.

Aidha, imekusanya Sh. trilioni 12.33 kuanzia Julai hadi Novemba, mwaka huu, ikiwa ni zaidi ya lengo lililowekwa kwa asilimia 105. Katika kipindi hicho, TRA ililenga kukusanya Sh. trilioni 12.30.

Kamishna Mkuu wa TRA, Yussuf Mwenda, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwenye mafunzo namna mamlaka inavyofanya kazi zake.

Alisema mamlaka imetengeneza stempu zenye alama nyingi za ulinzi ili kukabiliana na bidhaa bandia hasa vinywaji.

"Tumetengeneza stempu mpya zenye alama za ulinzi ambazo si rahisi kuzinakili. Hii tunaamini itatuongezea mapato na itapunguza tatizo la bidhaa feki hasa pombe sokoni," alisema.

Alisema TRA inaendelea kutoa elimu na kufuatilia kwa wafanyabiashara wasiotumia stempu sahihi, ili kudhibiti pombe feki.

Kuhusu makusanyo, alisema ni ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana. Katika kipindi hicho, TRA ilikusanya Sh. trilioni 10.80.

Alisema makusanyo hayo yamechangiwa na mamlaka kuongeza ufanisi na kuboresha uhusiano kati yake na walipakodi, yakiwamo mawasiliano na majadiliano na wafanyabiashara na ongezeko la walipakodi wapya.

"Tumeongeza Sh. trilioni mbili ndani ya miezi mitano, hii ni kazi kubwa. Tumejenga mazingira ya kuhakikisha walipakodi wanalipa bila kushurutushwa. Kipekee niwashukuru walipakodi wote," alisema Mwenda.

Alisema mapato ya forodha yameongezeka kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 kwa mwezi, hadi Sh. trilioni 1.2 na Sh. trilioni 1.15 Oktoba na Novemba mwaka huu, mtawalia.

Mwenda alisema ongezeko la mapato ya forodha limechangiwa na ufanisi katika bandari ya Dar es Salaam, baada ya kampuni ya DP World kuanza kazi, hasa suala la uondoshaji wa mizigo bandarini na kupungua kwa muda wa kuhudumia meli.

Mwenda alisema mamlaka hiyo inakusudia kuajiri watumishi 1,000 mwakani, ili kuongeza ufanisi hasa usajili wa walipakodi wapya.

Alisema kuanzia Januari mwakani, TRA itaanza kufanya makadirio ya tozo za forodha kwa mfumo mpya ambao utakuwa bora kuliko uliopo.

Alisema TRA inakusudia kuimarisha mifumo yake ili kuwezesha wafanyabiashara na walipakodi wengine, kupata huduma mtandao kwa uhakika na ndani ya muda mfupi.

Lengo, kwa mujibu wa Mwenda, ni kuongeza pato la taifa (GDP) kupitia kodi kutoka asilimia 13 ya sasa hadi asilimia 15.

Kuhusu matumizi ya risiti za kielektroniki, Mwenda alisema TRA imeimarisha mfumo wa ukaguzi wa mashine hizo kupitia mfumo wa EFDMS, ambayo inampa uwezo mtumishi wa mamlaka hiyo, kuona mfanyabiashara ambaye hajatoa risiti kwa muda mrefu na kuwasiliana naye ndani ya mfumo.

"Kwa hiyo kutosikia malalamiko sio kwamba hatukagui. Tumebadilisha staili, tunakwenda moja kwa moja kwa mhusika wanaangalia ni kina nani ambao hawatoi kabisa anafuatwa yule ndani ya mfumo kuulizwa kwa nini hatoi risiti na hii inatusaidia kuondoa malalamiko," alisema.

Hata hivyo, alisema TRA inakabiliwa na changamoto za baadhi ya wafanyabaishara kukwepa kodi pamoja na ukosefu wa mashine za ukaguzi katika mipaka ya Tunduma upande wa Zambia, Kasumulo na Namanga, inayochangia msururu mrefu wa malori yanayovuka kwenda nchi jirani.

"Mfano, kuna watu wanaanzisha biashara ili auze risiti za EFD, tumetengeneza kitengo kizuri cha uchunguzi, tunasaidiwa na vyombo vya ulinzi kuwabaini. Tukiwabaini tutarejesha kodi yetu yote na riba, pia tutawashitaki. Niwakumbushe wafanyabiashara, hakuna biashara ya kuuza risiti. Timu iko mtaani inafanyakazi na hivi karibuni kutakuwa na matokeo makubwa sana," alisema.

Alisema changamoto nyingine ni magendo kwenye mipaka ya nchi, inayochangiwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa vya ukaguzi mizigo mipakani.

Alisema katika mpaka wa Tunduma, wamekubaliana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), kusaidia kununua mashine upande wa Nakonde Zambia, ili kuondoa foleni ya malori Tunduma.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, aliielekeza TRA kuanza na mpaka wa Namanga, mkoani Arusha ili kuendana na kasi ya huduma inayotolewa upande wa Kenya.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Oran Njeza, aliipongeza TRA kwa kuongeza makusanyo ya mapato na kueleza kuwa Bunge linatamani kuona ongezeko la mapato litakaloiwezesha serikali kupunguza kukopa.

"Ushauri wetu wa muda mrefu ni kwamba TRA iwekeze kwenye mifumo ambayo inasomana ili kuongeza mapato. Tunaamini kwamba mifumo ikiwa mizuri, hiki kinachokusanywa kitaongezeka hata mara mbili.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga / WhatsApp : +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# Viongozi wa dini wajitwisha jukumu kuzuia ndoa utotoni

**Na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI wa dini wamesema wako tayari kutumia majukwaa yao kukemea ndoa za utotoni nchini.

Wamesema wako tayari kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu na uwezeshaji wasichana na kwamba kila msichana ana haki ya kulindwa dhidi ya ndoa hizo za utotoni.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam juzi wakati wa warsha iliyoshirikisha wadau mbalimbali wa kutetea haki za wasichana, viongozi hao wa dini walisema vitendo hivyo si vya kufumbia macho kwa kuwa vinasababisha athari mbaya kwa kundi hilo.

Sheikh Khamis Mataka aliomba serikali kuboresha sera na sheria ya ndoa, ili kuwalinda zaidi watoto wa kike ambao ndio waathirika wakubwa.

Hafla hiyo iliandaliwa na Msichana Initiative, Norwegian Church Aid (NCA) na Kamati ya Kudumu ya Madhehebu ya Haki za Kiuchumi na Uadilifu wa Uumbaji (ISCEJIC) kwa lengo kutambua umuhimu wa viongozi hao wa katika kuendeleza mapambao dhidi ya usawa wa kijinsia.

Sheikh Mataka alisema kuna haja ya serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ili kuzuia watoto wasiolewe katika umri mdogo.

"Hata maandiko ya kidini yanasisitiza kwamba ndoa inapaswa kuwa muungano wa heshima na wa hiari, si kulazimishwa kwa mtu yeyote," Sheikh Mataka alisema.

Mchungaji Monica Lugome wa Baraza la Kikristo Tanzania (CCT), aliweka msisitizo kwa kanisa katika malezi bora ya mtoto kuhakikisha kuwa haki ya kila mtoto ya kupata elimu na maisha yenye kuridhisha inaheshimiwa.

"Kama viongozi wa dini, ni wajibu wetu kuongoza jumuiya zetu kuelekea haki na uadilifu. Ni wakati wa kukomesha mila potofu za ndoa za utotoni na kumpa kila msichana fursa ya kufikia ndoto zake," alisema.

Alisema upo umuhimu wa kuhakikisha wanaoingia katika ndoa ni watu wazima ambao tayari wamepevuka kukabiliana na ugumu wa changamoto mbalimbali na siyo watoto.

"Kulazimisha watoto kuingia katika ndoa kunawanyima haki muhimu za elimu na maisha yenye kuridhisha, kwani wanaelemewa na majukumu mazito ya kujenga familia katika umri mdogo," alisema.

Sarah Shija ni Meneja Mipango wa NCA, alisema kukomesha ndoa za utotoni italeta mabadiliko makubwa katika uelewa kwa umma na mabadiliko ya kudumu kwa wasichana wa kitanzania.

"NCA wanaona kwamba bado kunahitajika juhudi ya kuleta mabadiliko chanya ya kijamii na kitabia, kuongeza ufahamu, na kuhamasisha jamii kuheshimu na kudumisha haki za watoto hasa wasichana ambao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali," alisema.

Mtaalamu wa Programu ya Upatikanaji Haki kwa Wanawake wa UN Women Tanzania, Rachael Boma, alisema ni jukumu muhimu la viongozi wa kidini kuwalinda watoto na kuunda kanuni za kijamii na kitamaduni zinazoweza kusaidia kuzuia ukatili.

"Viongozi wa kidini ni watu wanaoaminika katika jamii zao, wana nafasi ya kipekee ya kukuza ustawi wa watoto. Wanaweza kuzungumza dhidi ya mila mbaya kama vile ukeketaji, unyanyasaji, na kutelekezwa," alisema Boma.

Alisema pamoja na kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa katika kushughulikia suala hilo, bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kutokomeza kabisa ndoa za utotoni kwa kurekebisha sheria zilizowekwa ili zitamke kwamba umri wa kuolewa ni kuanzia miaka 18.

Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, Rebecca Gyumi, alisema kuna umuhimu mkubwa kuwashirikisha viongozi wa dini katika mapambano dhidi ya ndoa za utotoni.

"Kwa kuweka vita dhidi ya ndoa za utotoni kama suala la kimaadili na kidini, tunaamini itasaidia kuhamasisha mabadiliko ya kitamaduni ili kuhakikisha mtoto wa kike au msichana analindwa dhidi ya ndoa hizo za utotoni na anapatiwa haki zake za msingi," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Mawakili watakiwa kufika mahakamani na nyaraka za kuthibitisha walikokuwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imemtaka Mawakili wa Utetezi Edward Chuwa na Gabriel Mnyele wawasilishe nyaraka mahakamani kuonesha kwamba walikuwapo Mahakama Kuu baada ya kushindwa kufika mahakamani bila kutoa taarifa.

Pia imewataka wafuate sheria kwa kuwa wao ni wakongwe katika sheria. Wanajua taratibu zote ili mahakama isifanye kazi kama waganga wa kienyeji.

Hayo yaliagizwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya wa mahakama hiyo katika kesi ya tuhuma za kujeruhi na kutoa lugha ya matusi inayomkabili Bharat Nathwan (57) na mke wake, Sangita Bharat (54).

Hakimu Lyamuya alifikia hatua hiyo baada ya mshtakiwa Nathwan kueleza mahakama kwamba amepata taarifa kutoka kwa wakili wake Chuwa kwamba yuko Mahakama Kuu mbele ya Jaji Hemed na pia Mnyele yuko safari mkoani Dodoma kwa ajili ya kikao cha mahakama.

Baada ya Nathwan kudai hayo, Wakili wa Serikali Faraji Ngukah alidai hawana pingamizi na taarifa hiyo ya mawakili, lakini ni taratibu za mahakama kwamba kama mtu anapata udhuru, anatakiwa awasilishe mahakamani nakala ya wito.

> **“Wanatakiwa wafuate sheria, wafuate utaratibu, hivyo wanatakiwa walete vielelezo, leo (jana) hawapo. Siku ya kesi wavilete kuonesha kwamba walikuwa huko,” alisema Hakimu Lyamuya.**

“Kama huyu tunaelezwa yuko Dodoma, basi nyaraka ilitakiwa ioneshe hivyo ili mahakama ijiridhishe kwamba mawakili hawa wako Mahakama Kuu, kwa hiyo siku ya kesi wanatakiwa kuleta ushahidi.

“Si kama hatuwaamini, lakini tangu mwanzo hawa wenzetu wamekuwa na shida hii, ni kama wanapoteza muda wa mahakama. Tunaomba mahakama itoe maelekezo juu ya hili,” alidai Ngukah.

Pia alidai ametoka Mahakama Kuu kwenye kesi ya tuhuma za ugaidi Na. 61 ya mwaka 2022; Jamhuri dhidi ya Mbwana Puga, mbele ya Jaji Mtema, amewaacha wenzake wanaendelea. Yeye amefika mahakamani kwa ajili ya kesi hiyo kwa kuonesha uzito.

Alidai wana shahidi mmoja na walikuwa tayari kuendelea kusikilizwa kwa kesi kwa kuwa washtakiwa wote wawili walikuwa mahakamani.

Hakimu Lyamuya akawauliza washtakiwa kama wamemsikia Wakili Ngukah na kumwelewa. Mshtakiwa Nathwan alidai amesikia na amemwelewa vizuri kwamba mawakili wanapokwenda mahakamani, wanatakiwa wawe na vielelezo kuonesha walikuwa Mahakama Kuu.

“Sikiliza nikwambie, mawakili wako walipaswa kuyajua haya yote na si kwamba hawajui, wanajua vizuri kwa sababu ni wakongwe kwenye sheria. Kama hawako mahakamani, wanatakiwa walete taarifa, wasipoleta ni kama waganga wa kienyeji.

“Wanatakiwa wafuate sheria, wafuate utaratibu, hivyo wanatakiwa walete vielelezo, leo (jana) hawapo. Siku ya kesi wavilete kuonesha kwamba walikuwa huko,” alisema Hakimu Lyamuya.

Wakili Ngukah aliomba mahakama kwamba siku nyingine likitokea suala kama hilo, basi kesi iendelee kusikilizwa bila kuwapo mawakili, lengo ni kumaliza kesi mapema.

Kesi imeahirishwa hadi Desemba 10, 2024 saa sita mchana kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya India wanaoishi mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam wanatuhumiwa kwa mashtaka manne waliyoyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa Nathwan Julai 21, 2023, akiwa eneo la mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, ndani ya wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, kinyume cha sheria alimsababishia madhara makubwa Kiran Lalit kwa kuzamisha kichwa chake katika ndoo ya saruji iliyokorogwa.












REPUBLIC OF KENYA

KENYA HIGH COMMISSION IN DAR ES SALAAM, TANZANIA

**INVITATION TO TENDER FOR RENOVATION OF BUILDINGS**

**TENDER NO.: KHCD/OT/001/02/2024-2025**

The Kenya High Commission invites interested **“Bidders”** for **renovation of Government Properties in Dar es salaam** whose details are given below.

| S/NO. | PROPERTY TO BID | OTHER IMPORTANT INFORMATION | PHYSICAL LOCATION OF PROPERTY | DEADLINE FOR SUBMISSION |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Harambee Plaza Building | Located on Plot No. Plot 1858 Oysterbay and housing KCB Bank Tanzania Ltd | Ali Hassan Mwinyi Road/ Kaunda drive Junction | Friday 20th December 2024 at 15:00 Hours. |
| 2. | Kenya House (The Chancery) | Located on Plot No. Plot 1859 Oysterbay and housing The High Commission offices | Kaunda drive / Bongoyo Road Junction | Friday 20th December 2024 at 15:00 Hours. |

**ALL BIDS MUST BE SEALED, ADDRESSED AND SUBMITTED TO:**
**The High Commissioner**
**Kenya High Commission in Dar es Salaam**
**Kaunda Drive/Bongoyo Road Junction, Oysterbay**
**P.O. Box 5231, Dar es salaam, Tanzania**

So as to be received on or before **Friday, 20th December 2024 at 15:00 hours**. The sealed envelope should clearly be marked **“Bid for Renovation of Government Properties.”**
Requirements to Bid.

1. Tender documents to be collected from the Kenya High Commission offices upon payment of a non-refundable fee of TZS 115,000.00 banker’s cheque payable to the **“KENYA HIGH COMMISSION.”**
2. The bids should be submitted on working days between 10:00hrs and 15:00hrs.
3. Interested bidders may obtain further information in writing from the Kenya high Commission.
4. Appointments for site inspection of the properties and Pre-tender meetings to be done after this advert between 10:00hrs and 15:00hrs at their own cost.
5. The tender, as well as all correspondence and documents relating to the tender exchanged by the tenderer and the Procuring Entity, shall be written in English Language.
6. Bids submitted after the set deadline will not be considered.

KENYA HIGH COMMISSION
DAR ES SALAAM, UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

218279802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mazingira tuyatunze, yatulinde na maafa

**UCHAFUZI** wa mazingira umeleta athari kubwa katika mabadiliko ya tabianchi, hali iliyosababisha baadhi ya maeneo kukosa mvua na kuleta upungufu wa mvua.

Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeshuhudiwa katika baadhi ya maeneo ambako mvua imenyesha kupita kiwango na watu kukosa makazi na hata kusababisha vifo.

Umuhimu wa kuhifadhi mazingira unatakiwa uanzie katika ngazi ya familia na kupanua wigo hadi kwa wadau mbalimbali.

Watu muhimu na wanaosikilizwa katika jamii ni viongozi wa dini ambao Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliwahi kusema kuwa wanayo nafasi kubwa na kuwataka iwe ajenda maalum katika ofisi za umma, za binafsi au kwenye taasisi.

Umuhimu wa jamii kushiriki katika uhifadhi mazingira ni kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuendelea kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Aidha, jitihada ambazo Rais Samia amezichukua ili kuhakikisha suala la nishati safi linakubalika ni kukataa kukata miti na kuhamasisha kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Rais Samia amekuwa kinara wa nishati na alienda nchini Ufaransa kuhutubia kuhusu nishati safi na yeye akiwa ni Mwenyekiti mwenza wa mkutano huo, jambo ambalo ni ni fahari kwa nchi ya Tanzania.

Wajasiriamali wamepewa fursa kuanzisha biashara ya kuuza mitungi na majiko ya gesi hadi kwenye ngazi ya vijiji ili nishati hiyo iweze kupatikana kwa urahisi hali ambayo itaweka ukomo wa matumizi ya mkaa na kuni nchini.

Pia, serikali imechukua hatua za kisera na kimkakati ili kuleta matokeo chanya zikiwamo za kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Kutungwa kwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2014; kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032; kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021 hadi 2026; na kutungwa kwa Kanuni na Miongozo inayohusu masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Wizara inayosimamia mazingira imetakiwa ishirikiane kwa karibu na wizara za kisekta kuhakikisha maadhimisho mbalimbali ya kitaifa yanayogusa masuala ya mazingira yanatumika kikamilifu kuwezesha jamii kupata uelewa na kuweka alama za kudumu na matokeo yanayopimika kuhusu utunzaji mazingira ikiwamo Siku ya Upandaji Miti, Siku ya Hali ya Hewa, Siku ya Maji, Siku ya ardhi Oevu, Siku ya Mazingira na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni.

Uhamasishaji kuhusu utunzaji wa mazingira, Waziri Mkuu amezitaka ofisi za mikoa na wilaya, zisimamie suala hilo na kusisitiza kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira na ikibidi watumie mitandao ya kijamii kusambaza elimu hiyo.

Hiyo itasaidia kuongezeka kwa ufahamu miongoni mwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kutasaidia kupunguza uharibifu na kuimarisha usimamizi wa mazingira.

Aidha, elimu ijumuishe matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira ikiwamo matumizi bora ya ardhi, maji na nishati ili kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinabaki kuwa za kudumu kwa vizazi vijavyo.

Utunzaji wa mazingira unaanzia nyumbani kwako, sehemu yako unayofanyia shughuli za kukuingizia kipato na hata barabarani unapopita.

Kila mmoja anapoona mwenzake akiharibu mazingira ana jukumu la kumkemea ili ajue kuwa anachokifanya kinaathiri jamii na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Shule zinapofungwa familia zisijisahau

**SHULE** za msingi na sekondari zinakaribia kufungwa kuanzia wiki hii suala la kusoma, kufurahia likizo, masomo pamoja na kufaulu bado ni kipaumbele.

Usalama wa watoto na ulinzi wao ni jambo linalohitajika na ndilo la msingi kwa kila kitu, wazazi, walezi na jamii kumbukeni kulipa umuhimu wa kipekee.

Ulinzi na usalama unamgusa kila mmoja ili kuwaangalia watoto au wanafunzi kuanzia shuleni wanaposoma, mitaani wanapokaa na mambo muhimu wanayohitaji ili kuwasaidia wasome salama wakati huu wakiwa likizo yenye sherehe na matukio mengi.

Ni kwa sababu watoto wengi wanaoathirika na ukatili wa kijinsia hasa mabinti kupewa mimba, kutumiwa kingono na walimu au walezi ama wazazi, kadhalika wasichana na wavulana kuingiliwa kinyume cha maumbile, yote hayo yanachangiwa na kukosekana ulinzi na jamii kuwapuuza.

Ukiangalia zaidi eneo la kuendelea na maandalizi ya elimu ya sekondari hasa wanaomaliza msingi kila mmoja anatafuta kuwasaidia akiwaalika kujisajili na 'pre-form one' ili iwe rahisi wanapofika sekondari kuelewa masomo kwa wepesi. Hatukatai.

Wanachojifunza ni masomo ya kidato cha kwanza hasa Kiingereza kwa kiasi, huko nako kuna udanganyifu.

Watoto wanaweza kulazimishwa kufanya mambo ya kihalifu mitaani kwa kisingizio kuwa wamekwenda shuleni lakini wakatumbukia kwenye mikono ya wanyanyasaji.

Familia zikumbuke kuwa kusoma hiyo 'pre form one'pasipo na chakula kunamaanisha njaa isiyovumilika, matokeo yake ni mabinti kufanya lolote bila kujali itakuwaje ili wapate chakula, wasife njaa.

Yote hayo na mengine mengi huchangia mimba, unyanyasaji na watoto kutumiwa vibaya wakati huu wa likizo lakini pia wakiendelea kujifunza.

Ni vyema wazazi, walezi na wadau wa elimu watatue matatizo hayo yanayohusisha chakula na ulinzi ili kupunguza matatizo hasa kuwaumiza watoto ambao mara nyingi hawana hatia.

Usalama na ulinzi wa watoto unakwenda mbali zaidi kwa kuwasimamia na kuwaepusha na athari za utandawazi ni kwa sababu umewaharibu wawe wa msingi au sekondari kwa vile wakati huu wa likizo wanaweza kutumia muda mwingi kuangalia mitandaoni kujifunza'maovu.'

Wapo wenye simu janja na kompyuta wanaozitumia kuangalia maovu mitandaoni kama picha za ngono kwenye YouTube zenye maudhui yasiyo na maadili.

Wanajifunza masuala mengine makubwa kuliko umri wao, wapo wanaojifunza na kufanya uhalifu, kutumia dawa za kulevya, kuua na hata kudanganya.

Utandawazi unawatumbukiza katika kupenda muziki wa disko usiku na kuchochea watoroke nyumbani.

Wapo wengine kwa kuzoea maovu ya mitandaoni wanakimbilia kwenye sinema zinazoonyeshwa kwenye vibanda umiza mitaani.

Watoto hawa wanapokosa uangalizi wanaweza kuishi kwenye nyumba za sinema mchana au vibanda umiza, mabinti wanawaweza kuzamia huko wakawa waathirika wa unyanyasaji kwenye likizo.

Ikumbukwe kuwa kama familia na jamii hazitawajali watoto wakati huu wa likizo wengi wanaweza kushawishiwa na kutumbukia kwenye vitendo vya kuwakwamisha kimasomo.

Watoto wanaingia mitegoni wanapokwenda kwenye mabanda yanakoonyeshwa video asubuhi na mchana na kukutana na watu wanaowalipia kiingilio, kuwapa chips na soda kitakachofuata ni ulaghai na hadaa zinazoweza kuwaondoa shuleni kwa sababu za unyanyasaji kijinsia.

Pamoja udanganyifu huo wakati mabinti wanaweza kuingizwa mtegoni na walimu ambao ama kwa kisingizio cha kuwafundisha 'twisheni au pre form one' wanawabaka au kuwashawishi kuingia kwenye ngono.

Ni vyema kuwaangalia watoto wasiwe waathirika wa kutafuta fedha za kujikimu kwa kulazimishwa kufanyakazi za kuosha vyombo, kutafuta kuni, kufua nyumbani kwa walimu na watu wengine iwe mijini au vijijini.

Wazazi na wanafamilia walindeni watoto wasichwe au kusafirishwa kwenda kwa jamaa zenu mikoani kwa mjomba, baba mkubwa au bibi na babu kwa sababu huko nako si salama.

Kaeni na watoto wenu likizo maana hasara za kuwapeleka mbali na familia ni kubwa zaidi kuliko mnavyowaza.

TANGAZO

BONDI YANGU
Uwekezaji Wenye Tija

AZANIA BANK
Benki Inayozidi Matarajio

# WEKEZA SASA,

## Kuanzia TZS 500,000

Ofa itafungwa 06/12/2024

Riba ya **12.5%**
Kwa mwaka, itakayolipwa kila miezi mitatu

| PANDO | JUMLA YA FAIDA MIAKA 4 | KILA MIEZI MITATU |
|---|---|---|
| 500,000 | 250,000 | 15,625 |
| 10,000,000 | 5,000,000 | 312,500 |
| 50,000,000 | 25,000,000 | 1,562,500 |
| 100,000,000 | 50,000,000 | 3,125,000 |
| 1,000,000,000 | 500,000,000 | 31,250,000 |

*Fedha ya Pando italipwa baada ya miaka 4*




* *Waraka wa matarajio wa toleo hili la Hati fungani umeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)*

0800 110210
www.azaniabank.co.tz

218280802



Mkuu wa mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (kulia), akizungumza na baadhi ya wagonjwa waliofika kupata huduma za afya katika Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, mjini Musoma juzi, wakati wa kupokea madaktari bingwa 45 waliokwenda kuweka kambi hospitalini hapo, ili kutoa huduma za kibingwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia: Serikali inathamini mchango wa Jukwaa la Wakurugenzi Watendaji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali inathamini mchango wa jukwaa la Wakurugenzi Watendaji (CEO Roundtable -CEOrt) katika kuchangia jitihada za kujenga uchumi endelevu na unaostawi hapa nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia katika hafla CEOrt 2024 Dinner Gala) Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango alilipongeza jukwaa hilo na washirika wao kwa juhudi zao za kuendeleza maendeleo ya kijamii na kiuchumi hapa nchini.

"Nawaletea salamu za heshima kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye hakuwapo hapa leo kwa sababu ya majukumu mengine, lakini ameniagiza niwasilishe shukrani zake kwenu za dhati kwa mazuri mnayoyafanya," alisema.

"Rais anathamini michango yenu isiyokuwa na kikomo na kujitolea kwenu katika kujenga uchumi endelevu kwa kuwahusisha wadau mbalimbali wa sekta ya umma na sekta binafsi."

Dk. Mpango alielezea furaha yake katika juhudi za CEOrt zinazohusiana na masuala mbalimbali ikiwamo mazingira ya biashara na maendeleo ya rasilimali watu.

Alisema kaulimbiu ya usiku wa sherehe hii hizo za CEOrt mwaka huu inayosema "2050... Twende!" Kujenga Uchumi Uliostawi, Jumuishi, na Endelevu, na kusema kwamba inahusiana na Malengo ya Serikali ya Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050, ambayo ni kuifanya Tanzania kuwa taifa lenye uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2050.

"Tunahitaji kuendelea kuzingatia masuala muhimu kama mabadiliko ya tabianchi na kutathmini athari zake kwenye mazingira ya biashara," aliongeza Dk. Mpango.

Akielezea ushiriki wake hivi karibuni kwenye mkutano wa COP 29, alisisitiza ahadi ya Tanzania katika malengo ya kimataifa ya tabianchi na kusema ni muhimu kujenga uchumi imara licha ya changamoto za tabianchi.

"Kwenye hotuba yangu katika COP 29, nilisema kwamba mabadiliko ya tabianchi yanapunguza hadi asilimia 2-3 ya Pato la Taifa la Tanzania kila mwaka na kuleta hasara ya mabilioni ya shilingi," alisema Dk. Mpango.

"Inafurahisha kuona kuwa CEOrt pia ina juhudi za kuhamasisha biashara kujiunga na ajenda ya tabianchi."

Dk. Mpango aliwahimiza wanachama wa CEOrt kuendeleza juhudi zao kwa kubuni suluhisho bunifu na kuanzisha ushirikiano ambao utasaidia biashara kuendana na malengo ya tabianchi ya Tanzania na kunufaika na fursa zitakazotokana na hilo.

Makamu wa Rais pia alisisitiza uwekezaji unaoendelea wa serikali katika sekta muhimu za miundombinu kama vile barabara, reli, maji, usafiri wa angani, na nishati, ambazo zote ni muhimu kwa ukuaji na maendeleo ya uchumi.

"Tunahakikisha kuwa tunaboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kutekeleza sera zinazochochea sekta binafsi yenye ushindani," alisisitiza. "Hii ni pamoja na kurahisisha michakato ya usajili wa biashara, kupunguza vikwazo vya kisheria, na kuanzisha vituo vya kutolea huduma katika dirisha moja ili kupunguza urasimu na kupambana na rushwa."

Aidha, Tanzania inajipanga kuwa mchezaji muhimu katika masoko ya kikanda na kimataifa, kuvutia uwekezaji na kuchochea ukuaji.

Kwa upande wa maendeleo ya kijamii, Dk. Mpango alielezea mafanikio muhimu katika maeneo kama usalama wa chakula, elimu, huduma za afya, na usawa wa kijinsia.

Alisema kuwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi kimefikia asilimia 97 kufikia mwaka 2022, upatikanaji wa huduma za afya umeimarika na kuleta kupungua kwa vifo vya kinamama na watoto wachanga na uwakilishi wa wanawake katika elimu na nafasi za uongozi umeongezeka.

"Sekta binafsi imekuwa na mchango muhimu katika mafanikio haya na ni muhimu kwa kila mmoja wetu kuendelea na juhudi zetu, kuchukua jukumu la uwajibikaji, na kuonesha uzalendo katika kutekeleza majukumu yetu," alisema. "Pamoja, tunaweza kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050."

Dk. Mpango alisisitiza ahadi ya serikali kuimarisha ushirikiano wa umma na sekta binafsi, ambao ni muhimu kwa kukuza maendeleo ya taifa na uchumi.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa CEOrt, Santina Benson, alisema jukwaa hilo linajivunia hatua mbalimbali za maendeleo ikiwamo kuitisha majukwaa ya kujadili maendeleo ya kiuchumi, kupitia sekta za viwanda na biashara.

"Miaka hii imekuwa ya mabadiliko makubwa kwa CEO Roundtable, kwani tumepiga hatua kubwa katika maeneo yetu muhimu ya kipaumbele na kuendelea kutumia jukwaa la CEOrt kuanzisha mijadala juu ya masuala muhimu kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi ya nchi," alisema.

Aliongeza kuwa CEOrt imeendelea kufanya juhudi za kukuza uchumi kupitia sekta mbalimbali kama vile nishati, mipango ya urithi wa biashara za familia, maendeleo ya rasilimali watu, fursa za usafirishaji na umuhimu wa uchambuzi wa data katika kukuza maendeleo ya Tanzania.

Katika sherehe hiyo, watu kadhaa mashuhuri walitunukiwa tuzo kwa michango yao ya kipekee kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania, akiwemo aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Hayati Lawrence Mafuru.

# BoT yashtushwa kiwango cha watu wazima kutumia benki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema asilimia 10 pekee ya watu wazima mkoani Singida ndio wanaotumia huduma za benki, kiwango kinachoelezwa kuwa chini ikilinganishwa na cha kitaifa ambacho ni asilimia 22.

Kaimu Meneja msaidizi sera na chambuzi za huduma za kifedha kutoka BoT, Edmund Mbokosi alisena hayo jana katika kikao cha kujadili changamoto za kifedha na utatuzi wake Mkoa wa Singida ambacho kimewashirikisha Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na mameneja wa benki zinazotoa huduma za kifedha mkoani hapa.

Alisema katika huduma za kifedha Mkoa wa Singida wanatumia asilimia 50 wakati wastani wa kitaifa ni asilimia 72, bima ni asilimia tano, huduma za vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) Singida ni asilimia saba wakati lengo la kitaifa ni asilimia 12.

Mbokosi alisema kutokana na changamoto hiyo BoT imeamua kuja kutoa elimu ili kuangalia upandishaji kiwango cha matumizi ya huduma za kifedha katika Mkoa wa Singida kwa lengo la kuufanya mkoa kupanda kiuchumi na kuondoka katika nafasi ya tatu kutoka mwisho.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema mkoa utajitathimini kwenye sensa kwa kupita kwenye maeneo mbalimbali kama kwa wanafunzi shuleni na vyuo vilivyopo mkoani hapa ili kupandisha kiwango cha huduma za benki.

"Tuna vyuo vingi na taasisi nyingi na karibu kila mtu anatakiwa kulipwa pesa kupitia benki na hivi sasa kuna huduma mpya mfano ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa hiyo nina imani kiwango acha asilimia 72 cha huduma za kifedha tutakifikia," alisema.

Awali, Mchambuzi masuala ya fedha kutoka BoT, Michael Mwaituka, alisema Benki imejipanga kuwasaidia wajasiriamali nchini kupitia Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (ECGS) pamoja Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SME-CGS).

Alisema lengo la kuwezesha sekta binafsi wenye miradi mizuri kupata mitaji kutoka kwenye benki na taasisi za fedha zilizosajiliwa chini na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha 2006, wanapokuwa na upungufu wa dhamana.

Mwaituka alisema kuwa BoT wanasimamia Mfuko wa Udhamini wa mkopo kwa niaba ya serikali ili kuwasaidia Watanzania kupata mitaji kuongeza uzalishaji, ajira, fedha za kigeni na Pato la Taifa kwa ujumla.

Alisema Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa kati una lengo la kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati wenye miradi mizuri, lakini wana upungufu wa dhamana, kupata mitaji kutoka kwenye benki na taasisi za fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu.

Alisema kuwa mfuko huo unatoa udhamini usiozidi asilimia 50 kwa mikopo kati ya Sh. milioni 50 hadi Shilingu bilioni moja itakayotolewa kwa kipindi kati ya mwaka mmoja hadi mitano.

Mwaituka alisema kwa upande wa Mfuko wa Udhamini wa mikopo kwa ajili ya mauzo nje ya nchi, umelenga kuwezesha wakopaji wenye miradi mizuri kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa na mauzo nje ya nchi, kupata mitaji kutoka kwenye benki na taasisi za fedha, wanapokuwa na upungufu wa dhamana.

Alisema kuwa udhamini wa mikopo katika mfuko huo hauzidi asilimia 75 kwa mkopo unaolipika ndani ya mwaka mmoja na asimilia 50 kwa unaolipika zaidi ya mwaka mmoja.

Mwaituka aliongeza kuwa lengo ni kusaidia sekta binafsi pamoja na wajasiriamali wadogo na wa kati wenye miradi mizuri, lakini wana upungufu wa thamani kupata mikopo kutoka benki au taasisi za fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu.

Alisema ili uweze kupata dhamana katika mifuko huo, mwombaji ambaye ni mjasiriamali akiwamo mvuvi au mkulima, anatakiwa kutuma maombi katika benki yake akiwa na andiko linaloelezea mradi wake.

Amefafanua kuwa benki au taasisi ya fedha itafanya tathmini ya mkopo huo kwa kuzingatia sera yao ya mikopo. Benki husika ikiridhia kumkopesha na ikathibitika kuwa hana dhamana toshelevu, benki hiyo itatuma maombi BoT kwa ajili ya kupata dhamana kwa ajili ya kumkopesha mteja wake.



## Sekta ya utalii yachangia 17% pato la taifa

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Nkoba Mabula, amesema sekta ya utalii imechangia asilimia 17 ya pato la taifa kutokana na fedha za kigeni.

Amesema pia kumekuwa na ongezeko la mapato yatokanayo na sekta hiyo hadi kufikia asilimia 31 ambapo kwa sasa imefikia Dola za Marekani bilioni 3.4 kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 kwa mwaka 2019.

Alisema hayo mkoani Arusha, wakati akifungua mafunzo ya kujenga uwezo wa wahifadhi wanaosimamia utalii katika Hifadhi za Misitu na Malikale uliowakutanisha wahifadhi wa misitu nchini.

Aidha, alisema kuwa lazima ziwepo juhudi za serikali katika kuongeza mvuto kwa vivutio vya utalii na kuboresha huduma hiyo ili kuwavutia watalii wa ndani na wa nje, ambapo alisema serikali imeendelea kuchukua hatua za makusudi ili kuhakikisha kuwa idadi kwa lengo la kufikia idadi ya milioni tano kwa mwaka 2025.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utalii Wakala wa Misitu na Uhifadhi, Dk. Thereza Mugobi, alisema mafunzo hayo yatawapa uwezo na ujuzi katika utekelezaji wa majukumu yao na nyenzo zilizozinduliwa zitumike vizuri ili kufikia lengo katika kuwafikia watalii wengi.

Alisema wanaendelea kufuatilia na kutoa ushirikiano ili kuhakikisha shughuli zinazofanyika hazikwami katika sekta ya utalii, huku akipongeza matokeo mazuri yanayotokana na juhudi za wahifadhi.

Naye Prof. Dos Santos Silayo alisema kuwa utalii katika misitu wageni wasiopungua 250,000 na mapato yasiyopungua Sh. bilioni 1.6 kwa mwaka ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 wanatarajia kupata wageni wasiopungua 300,000 na mapato yasiyopungua Sh. bilioni tatu.

Hata hivyo alisema wameweka mikakati ya kuhakikisha malengo yanatimia ambapo rasilimali fedha ni mojawapo ya jitihada wanazozifanya kuhakikisha bionoiai inaendelea kuwepo katika sehemu ya uhifadhi, lakini pia kuboresha miundombinu inaboreshwa.

Mhifadhi Mkuu kutoka TFS, Somen Mtereka alisema lengo la mafunzo hayo ni kujenga uwezo wa kusimamia na kuibua mazao mapya ya misitu kwa ufanisi ambapo wameandaa mada mbalimbali zitakazofundishwa kwa siku tatu.

# INEC: Wafungwa wa miezi sita gerezani wataandikishwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TUME Huru ya Uchaguzi (INEC) imesema wafungwa, wanafunzi wa vyuo vya mafunzo waliohukumiwa vifungo vya chini ya miezi sita pamoja na mahabusu, wataandikishwa kuwa wapigakura katika uchaguzi mkuu ujao.

Uandikishaji huo utafanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 15(2)(c) ya kanuni za uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura za mwaka 2024.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa INEC, Mtibora Seleman, alisema hayo katika mkutano wa wadau wa uchaguzi mkoani Kilimanjaro uliohusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura.

Seleman, alisema uboreshaji huo ni wa awamu ya kwanza kwa wadau, kwamba tume inaeweka utaratibu huo ili kuwapa wananchi haki ya msingi ya kupiga kura.

Alisema kutokana na utaratibu huo, kwa Tanzania kuna vituo vya kuandikisha wapiga kura 130 vilivyoko kwenye magereza na kwa Zanzibar kuna vituo 10 vilivyoko kwenye vyuo vya mafunzo.

Aidha, alisema kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, wapigakura 5,586,433 wanatarajiwa kuandikishwa sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699.

Alisema jumla ya wapigakura 4,369,531 watatarajiwa kuboresha taarifa zao.

Alitaka wadau kuwatumia wanahabari ili kutoa taarifa sahihi kuhusu uboreshaji wa daftari lakini pia kuepuka upotoshaji katika masuala yanayohusu tume.

"Ukitaka jambo liende kwa mafanikio au zoezi la uboreshaji wa daftari lifanikiwe tukae vyema na vyombo vya habari lakini pia wanahabari wasimamie taratibu katika utoaji taarifa kupitia vyanzo sahihi," alisema.

Alitaka Jeshi la Uhamiaji kuhakikisha wanaoandikishwa wawe ni raia wa Tanzania na siyo vinginevyo.

Mkuu wa Magereza Mkoa wa Kilimanjaro, Leonard Burushi, aliomba tume kutoa kanuni ambazo zitaongoza taratibu ili wale ambao watafungwa chini ya miezi sita lakini wakati wa kupiga kura watakuwa nje ya gereza.

Naye Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Basil Lema, alitaka mafunzo yaliyotolewa kwa wadau wa ngazi za mkoa zitolewe pia ngazi za chini za vyama vya siasa.

Alisema ni vyema vyama vikapata elimu ili kuhamasisha wanachama wake kujitokeza kuboresha taarifa zao.

Katika majibu yake kuhusu wafungwa na mahabusu chini ya miezi sita, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Tume ya Uchaguzi, Seleman alisema zipo kanuni zinazazoongoza kundi hilo na elimu itaendelea kutolewa.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi, Dk. Pindi Chana (wa tatu kulia), akabidhi malori matano na mitambo mitano vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.4, vilivyonunuliwa kupitia mradi wa dharura wa Uhifadhi na Utalii Tanzania kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Jenerali mstaafu George Waitara, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwakilishi wa Balozi wa Ujerumani nchini, Julia Knonbeg na (kulia) ni Naibu Kamishna wa Uhifadhi TANAPA, Massana Mwishawa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TVA: Madaktari tokomezeni magonjwa ya mifugo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MADAKTARI wa wanyama wametakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wanatokomeza magonjwa ya mifugo nchini, ili mifugo iweze kuuzwa nje ya nchi na serikali kuongeza pato la nchi.

Hayo yamo katika taarifa ya Mwenyekiti wa Chama cha Kitaaluma cha Kisayansi cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA), Prof. Esron Karimuribo, aliyoitoa wakati wa maandalizi ya kongamano la 42 la siku tatu la TVA linalotarajiwa kufunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Prof. Karimuribo, alisema kuwa katika miaka ya 1970 hadi mwaka 1980, mifugo ilikuwa ikikabiliwa na magonjwa mengi lakini hali hiyo imebadilika na magonjwa yote ya kuambukiza yametokomezwa, kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na madaktari wa mifugo.

Prof. Karimuribo alisema kuwa TVA imekuwa ikishirikiana na serikali katika kukabiliana na magonjwa ya mifugo na kufikia hatua sasa mifugo ya nchini kukubalika kuuzwa nje ya nchi na kuingizia serikali mapato na fedha za kigeni.

Aidha, aliishukuru serikali kwa uamuzi wake wa kuongeza bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi hadi kufikia Sh.bilioni 460 na hiyo inawapa nguvu wataalamu kufanya kazi katika mazingira mazuri yenye kuisaidia nchi kutoka ilipo na kusonga mbele.

Prof. Karimuribo ambaye ni Mhadhiri Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro alisema serikali imetenga Sh.bilioni 28 kwa ajili ya chanjo ya mifugo hiyo.

Katibu Msaidizi wa TVA kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Caroline Ulomi alisema chama hicho ni mmoja ya vyama vya kitaalamu vikongwe nchini na kinatambulika serikalini na kinaisaidia serikali, hususani Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika kupambana na magonjwa ya mifugo na kuthibiti magonjwa ya milipuko.

Ulomi alisema madaktari wa mifugo waliopo katika TVA wamesambaa nchini, ikiwemo Wizara ya TAMISEMI lengo likiwa ni kuhakikisha mifugo yote nchini inakuwa salama kwa maslahi ya nchi.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sayansi cha Nelson Mandela cha mkoani Arusha, Dk. Gabriel Shirima alisema kuwa ubora wa mifugo na wanyama ikiwa salama na afya ya binadamu inakuwa salama na uwezekano wa ongezeko la mifugo na wanyama ikawa kubwa na nchi kuongeza mapato.

Kongamano hilo linatarajiwa kuwa na washiriki zaidi ya 2,000 wa hapa nchini na wataalamu kutoka Jumuiya ya Madola.



## HABARI KANDA YA ZIWA

# 'Drones' kutumika kudhibiti uvuvi haramu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKURUGENZI wa Uvuvi nchini, Prof. Mohamed Shekhe, amesema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanatarajia kuanza kufanya doria kwa kutumia ndege zisizo na rubani ili kuweka usalama wa viumbe katika maji.

Prof. Mohammed alibainisha hayo juzi jijini Mwanza, katika mkutano wa kupokea maoni ya kuboresha kanuni za uvuvi pamoja na wadau wa sekta hiyo.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha uchumi wa bluu utakaokuwa na tija kwa mwananchi na taifa kwa ujumla, hivyo itahakikisha inadhibiti uvuvi haramu kwa kushirikiana na wadau.

"Tunaanzia na ndege tano na kwa Ziwa Victoria tutakuwa nazo mbili na hili zoezi litaanza mwaka ujao wa fedha, hatua hii itasaidia kutokomeza uvuvi haramu na kuwa na uhakika wa usalama wa viumbe maji," alisema Prof. Mohamed.

Aidha alisema sekta hiyo bado inachangia asilimia 1.8 katika pato la taifa kiwango ambacho ni kidogo kulinganisha na ukubwa wa uchumi utokanao na sekta hiyo, hivyo kutaja mkakati uliopo sasa kuwa ni kuhakikisha maboresho yenye tija yanafanyika.

Alisema maboresho hayo yanalenga kuvutia zaidi wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi, hasa baada ya kuwa na uhakika wa mazingira mazuri na wingi wa rasilimali zilizopo.

"Tumekuwa na utaratibu wa kuyafungia maziwa kwa muda hasa katika shughuli za uvuvi wa dagaa, tumeona namna zoezi hili lilivyokuwa na tija wanaporudi kuvua upatikanaji unakuwa wa kiwango kikubwa na soko linakuwa zuri," alisema Prof. Mohammed.

**Aidha utafiti huo haukupishana zaidi na ule uliofanywa na Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) mwaka 2005, ukieleza kuwa miaka 40 iliyopita mpaka kufikia mwaka huo aina 200 za samaki katika ziwa hilo wametoweka, huku sababu kubwa ikitajwa kuwa ni uvuvi haramu na uharibifu mkubwa wa mazingira**

Wakati huohuo, imeelezwa kuwa kupanda kwa bei ya samaki katika mikoa ya Kanda ya Ziwa imezidi kushamiri, huku uvuvi haramu ukitajwa kuwa sababu kutokana na kuvuliwa kwa samaki wasiokuwa na sifa.

Samaki ambaye alikuwa akinunuliwa kwa Sh. 3,000 hadi Sh.5,000 kwa sasa anauzwa kati ya Sh.10,000 hadi 15,000.

Njia mbalimbali za kudhibiti uvuvi haramu ikiwamo doria za askari, kuchoma nyavu na kukamatwa kwa mitumbi na wavuvi haramu zimeanza kutumia kuanzia miaka ya nyuma bila mafanikio.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Utafiti wa Mazingira la ACCORD Tanzania, mwaka 2021 ulibainisha kuwa ifikapo mwaka 2048 kutakuwapo na upungufu mkubwa wa samaki katika Ziwa Victoria, kutokana na uzalishaji samaki nchini kushuka kwa asilimia zaidi ya 50, kutoka tani 400,000 hadi tani 200,000, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Aidha utafiti huo haukupishana zaidi na ule uliofanywa na Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) mwaka 2005, ukieleza kuwa miaka 40 iliyopita mpaka kufikia mwaka huo aina 200 za samaki katika ziwa hilo wametoweka, huku sababu kubwa ikitajwa kuwa ni uvuvi haramu na uharibifu mkubwa wa mazingira.



Mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA), Mkoa wa Shinyanga, Rashidi Katabanya (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, mjini Shinyanga juzi, kuhusu chama hicho, kuridhishwa na uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Vijana UKIMWI bado upo, chukueni tahadhari'

**Na Waandishi Wetu**

VIJANA wanaoishi maeneo ya mipakani wametahadharishwa juu ya uwapo wa ugonjwa wa UKIMWI, huku wakitakiwa kuendelea kujilinda dhidi ya ugonjwa huo.

Mratibu wa UKIMWI kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Godfrey Mkenda, alitoa ushauri huo katika hafla ya Siku ya Ukimwi Duniani iliyofanyika juzi wilayani hapa.

Alisema licha ya maambukizi ya VVU wilayani humo kupungua kutoka asilimia 1.7 mwaka 2023 hadi 1.5 Novemba 2024 bado kundi la vijana wenye umri wa miaka kati ya 15 hadi 25 limeonekana kuwa hatarini zaidi.

"Tumefanya operesheni ya siku 14 kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa elimu juu ya kujikinga na UKIMWI na kuwafikia watu 5,000 ambao wamepata elimu ya kujikinga na ugonjwa huo ambapo asilimia 0.2 wilayani hapa wanatumia dawa za kufubaza, hivyo tumeendelea kukemea ngono zembe, kuacha ukeketaji na kujiweka kando na dawa za kulevya, " alisema Mkenda.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Tarime, Saul Mwaisenye, aliwataka wananchi kujitokeza kupima afya zao mara kwa mara na kuendelea kujikinga na maradhi yakiwemo ya UKIMWI.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Amini Vasomana, alisema siku hiyo ilianzishwa kutambua athari za janga la VVU/UKIMWI, kuelimisha watu na kutetea walioambukizwa ambapo utepe mwekundu ukawa ishara ya mshikamano kwa wale walioathirika.

**Imeandaliwa na Samson Chacha na Ambrose Waitangwa (TARIME).**

# Waomba mita za 'Luku' kumaliza malalamiko bili za maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama (KUWASA) kuwafungia mita za malipo ya kabla 'luku' zitakazosaidia kuondoa malalamiko ya ubambikizwaji wa bili ya maji kila mwezi.

Walitoa ombi hilo juzi katika kikao kazi cha kujadili rasimu ya mkataba wa huduma kwa wateja kati ya KUWASA na wateja wao.

Mkazi wa Kata ya Kagongwa, Ismali Masolwa, alisema wamekuwa na malalamiko ya ongezeko la ankara za maji kila mwezi na ili kuondoa adha hiyo ni vema mamlaka kuja na utaratibu mpya wa kuwafungia mita za luku.

Alisema, wasoma mita za maji wamekuwa wakisoma bila ushirikishwaji wa wateja kutambua kwa mwezi wametumia kiasi gani cha uniti za maji, badala yake wamekuwa wakipokea bili kwa njia ya simu ya mkononi hali ambayo imekuwa ikiibua malalamiko kuwa ankara hizo ni kubwa kulinganisha na matumizi waliyotumia.

Mkazi wa Kata ya Mhongolo, Joakimu Simbira alisema luku za maji ndiyo suluhu ya kumaliza malalamiko ya wananchi juu ya ongezeko la ankara za maji ya kila mwezi na kuishauri mamlaka hiyo wakati wa kusoma mita wahakikishe wanawashirikisha na siyo kusoma wenyewe.

Akitoa taarifa ya mamlaka hiyo, Ofisa Uhusiano, John Mkama alisema wanawateja 34,021 kutoka kata 17 kati ya 20 za Manispaa ya Kahama na kata moja ya Isaka-Msalala na utoaji wa huduma ni asilimia 84 na ni saa 24.

Akijibu hoja hiyo Mkurugenzi wa Kitengo cha Ununuzi KUWASA, Adam Mlagwa alisema wameshapokea maelekezo kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kubadilisha mita za zamani kwenda mita za kisasa za luku.

Alisema na sasa wapo katika majaribio na yatakapokamilika na kutoa matokeo watawaunganishia wateja wao.

Alisema mita hizo zimekuwa na changamoto nyingi ikiwemo ya kujifunga mara kadhaa hasa zinapoingiliwa na upepo, kuruhusu maji kutoka malipo yanapokwisha na wanaendelea maboresho yake.



Ukurasa 14

**SIKU 16 KUPINGA UKATILI SUMAIYA ABADALLA SHUJAA ALIYEUSHINDA MFUMO DUME**



Ukurasa 12

**SIKU 16 UKATILI Unyanyasaji unavyozidi kukithiri tuangalie sheria hizi ndio tatizo**



# Uchaguzi S/Mitaa utumiwe kuboresha ujao wa 2025

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI wa serikali za mitaa umemalizika huku CCM ikishinda kwa kishindo, lakini ingefaa changamoto na mafanikio yaliyoonekana vitumike kuboresha uchaguzi mkuu wa 2025.

Wakati CCM wakishangilia ushindi mnono, baadhi ya vyama vya upinzani vinadai havikuridhishwa na mchakato huo na kushauri serikali na wadau wa kisiasa kuutazama upya.

Malalamiko na madai ya upinzani yanachambuliwa na baadhi ya wadau wa kisiasa wanaozungumzia uchaguzi huo ambao upinzani uliambulia viti vichache kwenye mitaa, vijiji na vitongoji.

Miongoni mwa wadau hao ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala wa Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiwa, ambaye anasema uchaguzi huo umeonyesha jinsi ambavyo wasimamizi wa ngazi za chini wamebeza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutaka uamuzi wa wananchi kuheshimiwa.

"Kama utakumbuka, maelezo ya Rais Samia kabla ya uchaguzi huo yalikuwa ni kutaka uwe huru na haki na kwamba wananchi wasiingiliwe, wachague kiongozi wanayemtaka. Watu wengi walifurahia kauli yake watendaji wa chini wamekwenda kinyume," anasema Ngawaiya.

Anaeleza kuwa hayo yote yanatokana na uroho wa kupeana madaraka uliofanywa na watendaji hao ambao umesababisha waende kinyume na kile ambacho Rais alikuwa akikihimiza kila mara.

Ngawaiya anafafanua kuwa Rais hakutaka ubabaishaji katika uchaguzi huo, lakini badala yake yamejirudia yaliyotokea miaka ya nyuma ya wananchi kunyimwa uhuru wa kuchagua viongozi wanaowataka.



Wananchi wakiangalia majina yao ukutani kabla ya kupiga kura wakati wa uchaguzi wa viongozi wa Serikali ya Mtaa wa King'azi B, Kata ya Kwembe Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Kinachoendelea ni funika kombe mwanaharamu apite, kwani wenyeviti wapya wameshaapishwa. Kwa mazingira kama haya ni wazi kwamba bado tuna safari ndefu ya kufikia demokrasia tunayoitamani," anasema.

### UCHAGUZI URUDIWE

Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Doroth Semu, anasema uchaguzi huo unatakiwa kurudiwa, kwa maelezo kwamba mchakato mzima wa uchaguzi umevurugwa kwa kupora madaraka ya wananchi kuchagua viongozi wanaowataka bila kuingiliwa.

"Hivyo, matokeo ya uchaguzi huo yaliyotangazwa na TAMISEMI yafutiliwe mbali, badala yake urudiwe upya. Sisi kama chama hatukubaliani na matokeo hayo," anasema Dorothy.

Dorothy anasema wananchi kutoachwa huru wachague viongozi wanaowataka, ni sawa na kuwalazimisha, na kwamba mtindo huo hauwezi kusaidia nchi kufikia maendeleo.

Anafafanua kuwa kama kiongozi hakuwa chaguo la wananchi, hawawezi kumpa ushirikiano kuleta maendeleo na atashindwa kuitisha, mikutano, kwa ajili ya kuwasomea mapato na matumizi.

"CCM wasitambe kuwa wameshinda kwa kishindo, bali watafakari huo ushindi wao unaolalamikiwa una umuhimu gani kwa maendeleo ya nchi. Sisi tunataka uchaguzi wa serikali za mitaa urudiwe," anasema.

### ZIPO HASARA 3

Joseph Selasini, Makamu Mwenyekiti NCCR-Mageuzi Taifa (anayekataa kuhusisha maoni yake na chama), anasema uchaguzi huo utasababisha hasara tatu iwapo hakuna hatua zitakazochukuliwa za kuubatilisha ili wananchi wachague viongozi wanaowataka.

"Nianze kwa kukumbusha kuwa viongozi wa serikali za vijiji na mitaa ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi kwa kuwa karibu asilimia 70 ya bajeti ya nchi inapelekwa huko kwenye elimu, afya, miundombinu, kilimo, ufugaji na uvuvi. Viongozi hao ni muhimu kwa kuwa ndio wanaohamasisha ushiriki wa wananchi kwenye miradi ya maendeleo."

Selasini anasema wanawahamasisha kujitolea nguvu kazi kama kusomba maji, mawe, kuchimba msingi kujenga madarasa au ofisi ama shughuli zozote za kijamii.

"Kama viongozi hawakuchaguliwa na wananchi watashirikianaje na wale wanaowaongoza? Kama kuna malalamiko, serikali itafute jinsi ya kuyamaliza, isipofanya hivyo, tutakuwa tumemaliza uchaguzi, walioshinda wameshinda, lakini hasara itakuwa kubwa.

Hatuwezi kuziba masikio kuwa hakuna malalamiko, vinginevyo hakutakuwa na maendeleo. Hiyo ni hasara ya kwanza," anasema.

Kuhusu hasara ya pili, anafafanua kuwa mchakato wa bajeti unaanzia katika mitaa, vijiji na vitongoji na kwamba halmashauri ya ngazi hizo inaainisha mahitaji ya wananchi kisha wenyeviti ni wajumbe wa baraza la kata wanaopeleka vipaumbele vyao kwenye baraza ili kufikishwa kwenye halmashauri kwa utendaji zaidi.

"Baraza hilo ndilo linalokutinisha kata zote na kupeleka mahitaji katika kamati ya maendeleo ya wilaya, kisha mkoani hadi wizarani. Sasa kama kuna viongozi wasiojua wanafanya nini, hawawezi kuuliza wananchi wanataka nini, maana yake kwenye baraza la mtaa atakwenda kuwa sanamu na serikali itashindwa kupanga maendeleo ya eneo husika. Hiyo ni hasara ya pili," anasema.

Aidha, anafafanua kuhusu hasara ya tatu kuwa kuendelea kuwa na viongozi wa chama kimoja kunasababisha washindwe kuhoji lolote na hivyo kuchangia mambo kwenda ovyo ikiwamo ulaji wa rushwa.

"Hivyo, wajue kuwa mtaani kuna malalamiko kuhusu uchaguzi huo, kutoka hata kwa wanaCCM wenyewe. Kwa kuwa serikali ina masikio yake ambayo ni wananchi, isikie kilio chao ili kuondokana na hasara hizo tunazotarajia kuzipata kupitia uchaguzi huo," anasema Selasini.

Katika uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita Novemba 27 CCM, ilishinda kwa asilimia 98.8 ikizoa nafasi 4,213 katika nafasi za serikali za mitaa.

Kwa upande mwingine, chama kikuu cha upinzani, CHADEMA, kimeshinda nafasi 36 pekee, sawa na asilimia 0.84 ya jumla ya nafasi zilizogombewa.

Matokeo hayo yanakuja baada ya malalamiko kutoka kwa baadhi ya vyama vya upinzani, ambao wanakosoa mchakato mzima wa uchaguzi.

SIKU 16 UKATILI

# Unyanyasaji unavyozidi kukithiri tuangalie sheria hizi ndio tatizo

NA GAUDENSIA MNGUMI

UNYANYASAJI na ukatili kijinsia unaohusisha kutelekeza familia, vipigo, watoto kuozwa, kuingiliwa kinyume cha maumbile, mimba utotoni, kunyanyasa wanawake wenye VVU, kuua wazee kwa kusingizia wachawi ni tatizo mijini na vijijini.

Taarifa ya Jeshi la Polisi kuhusu ukatili wa kijinsia inaonyesha kuwa wanapokea malalamiko mengi kwenye madawati ya kijinsia na kwenye ripoti zinazofikishwa vituo mbalimbali.

Maelezo hayo yanayotolewa Julai mwaka huu yanaonyesha kuwa kuanzia Januari hadi Desemba 2023 matukio ya unyanyasaji kijinsia na ukatili yalikuwa 22,147 kwa watu wazima.

Wanawake walionyanyaswa walikuwa 13,322 wakati wanaume walikuwa 8,825 . Ripoti ya polisi inasema kuna ongezeko wakati mwaka 2022 kipindi kama hicho yalikuwa 18,403 ziada inaoneka 2023 kwa kuwa na matukio 3,744.

Ripoti inasema kuna ongezeko kubwa la unyanyasaji kijinsia kwa watoto mengi yakifanyika ndani ya familia na kwenye jamii pia. Yanahusisha kuuawa, unajisi- ulawiti, kubaka, mimba za utotoni na vipigo kupindukia.

Wakati huu dunia inaposisitiza haki kwa wanawake, wasichana na watoto inakumbusha kupinga ukatili kwa kuzingatia Siku 16 za Kupinga Ukatili Kijinsia, ukirejea kwanini ukatili unakithiri kuwepo mimba za utotoni licha ya jitihada za kutoa elimu kuhusu ulinzi wa watoto, kuwafundisha kujitetea na kujilinda sheria zinaendelea kuwa kikwazo.

Kwa hiyo mzizi ni sheria, kama ya ndoa ambayo inaruhusu binti wa chini ya miaka 14 kuozwa kwa kibali cha mahakama, mzazi au mlezi.

Licha ya Mahakama ya Rufani kuamuru vifungu 13 na 17 vya sheria hiyo virekebishwe bado serikali inakaa kimya wasichana wakiendelea kuathirika.

Sheria nyingine chanzo ni ya ajira na mahusiano kazini ya 2004 zote zinawanyanyasa watoto hasa mabinti na kusababisha kupata mimba, kudhalilishwa, kutosoma na hata kuuawa.

Sheria ya kazi ya 2004 inaruhusu watoto wenye miaka 14 kupata ajira na kufanyakazi nyepesi. Hizo kazi ni zipi ni nani anayesimamia? Ikumbukwe kazi ni kazi ukimruhusu mtoto akawe 'hausi geli' at 'shamba boy 'mjini hata kama ana miaka 14 lazima apitie magumu.

Sheria mathalani inasema watoto hawaruhusiwi kufanyakazi zaidi ya saa sita. Ni nani anayejua hayo akiwa nyumbani kwa mwajiri pengine yuko Arusha, Dodoma na familia yake iko Mtwara?

Sheria inaeleza ajira haramu ni ile inayomkwamisha mtoto kwenda shule, ni ile inayomwathiri mtoto kimwili na kisaikolojia. Inakuwaje watoto waruhusiwe kufanyakazi ambazo zinakiuka vigezo hivyo na walitakiwa kuwa shule?

Wakati mwingine sheria hizi zinachochea unyanyasaji watoto na kusababisha mimba, ndoa, ubakaji, ulawiti na utumikishwaji haramu kwenye mashamba ya tumbaku, mifugo na kilimo kwa ujumla.

Ipo sheria ya matunzo ya mtotto aliyezaliwa lakini baba na mama hawakufunga ndoa. Inamtazama zaidi mtoto lakini inaelekeza kiasi kidogo cha fedha kitolewe kulipia gharama za matunzo. Awali ilikuwa Shilingi 100 kwa siku, lakini baada ya marekebisho inaagiza mzazi mama kupewa Shilingi 3,500 kwa mwezi.

Kadhalika sheria hiyo haimjali wala kumzungumzia mama mtoto ambaye ametelekezwa.

Hiki ni kikwazo kwa sababu fedha hizo ni kidogo mno, 3,500 kwa siku ikichanganuliwa inanunua kipimo kimoja cha mkaa 2,000 na fungu la mboga Sh. 800 na mafuta kipimo kimoja mijini.

Ikumbukwe mama anahitajika kumhudumia mtoto asubuhi, mchana na jioni. Kadhalika analipa kodi ya nyumba ambayo ndogo ni Shilingi 20,000 kwa mwezi. Hivi kwa gharama hizo maisha ya mtoto yanakuwaje? Ni magumu bado hasa mijini.

Sheria ya Mtoto ya 2009 haijamgusa mama mzazi kwa kuzingatia sheria ya ndoa pale ambapo wazazi wametengana na kutalikiana, mtoto atakuwa na haki zake za msingi. Sura ya 26:1(a),(b),(c) inaongelea haki ya mtoto wazazi wanapotengana.

Hivyo upungufu mkubwa, mama anayetelekezwa, pamoja na mtoto wake hawajaunganishwa moja kwa moja kisheria.

Inaelekea sheria haimtambui mama mzazi ikumbukwe ametelekezwa kuwe na sheria za kumuwajibisha na kumwadhibu baba anayehusika na uvunjaji wa sheria ya kukataa familia yake.

Kwa kutumia mwanya au udhaifu huo wanaume hawajali kutelekeza wanawake ndiyo maana ukatili unazidi.

Watu wengi wanaipuuza sheria ya makosa ya kujamiiana ya mwaka 1998 maarufu kama SOSPA hutumiwa kuficha makosa na hata kujitajirisha.

Wapo baadhi wajanja wakisikia kuna mtuhumiwa kampa mtoto mimba wanaitumia kumweleza kuwa atafungwa miaka 30 au kama kanajisi mtoto mdogo ni jela maisha, hivyo wanatumia mbinu kuvuruga kesi na ushahidi ili wapatee fedha wayamalize na kuishirikisha familia ambayo inalipwa kiasi kidogo ili kukaa kimya.

Baadhi ya wachache wanaoweza kutumia mwanya wa 'umbumbumbu' wa sheria kuwa ni pamoja na viongozi wa vijiji au mitaa, mawakili, walimu shuleni na wana familia wenye tamaa ya fedha au mali.

Kwa kutumia udhaifu wa kupata pesa wahusika huongea na wazazi wa waathirika kisha kuchukua hela na kuwapa ujanja wa kukimbia na kukwepa kesi ikiwamo kukataa kutoa ushahidi.

Kutoa hela si jambo gumu ni rahisi kwenye jamii za wafugaji ambao wanaendekeza mila potofu hivyo wao kutoa ng'ombe 20 au hata Shilingi 1,000,000 ili kukwepa kesi hizo haisumbui.

Kwa ujumla kuumiza watoto kunachangiwa pia na kula rushwa na kusababisha mabinti kupewa ujauzito na kesi zao kuishia kinyemela baada ya watu kula mlungula.



Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi: **PICHA: MTANDAO**

**UTASHI WA KISIASA**

Ukosefu wa utashi wa kisiasa pengine ndicho chanzo kingine kuendeleza mfumo dume na unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa watoto.

Mfano serikali hata sasa haijarekebisha Sheria ya Ndoa ya 1971 licha ya Mahakama ya Rufani kuagiza baadhi ya vifungu kandamizi vifutwe.

Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini ni mwiba wenye ncha kali kwa ajira za watoto.

Wananchi wanatamani wanaonyanyasa watoto wakikamatwa na hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao. Lakin mara nyingi haki inachelewa, haionekane ikitendeka, hukumu zinachukua muda mrefu.

Rushwa nayo ni tatizo. Baadhi ya wahusika wasio waadilifu mitaani, vijijini, mahakamani, ndani ya jeshi la polisi hushirikiana kukwamisha kesi za kuzuia unyanyasaji watoto, mimba au ndoa za utotoni.

Ndiko kushirikiana na wazazi, walezi na watoto kumaliza kesi hizo baada ya kupewa kitu kidogo na kwa wengine huendelea kutolewa mara kwa mara, hivyo kupata pa kulia.

Wakati mwingine madawati ya jinsia yanakosa ofisi, mafunzo, vitendea kazi kama magari, kompyuta, 'printa' na kuendeshwa bila bajeti ni moja ya mambo yanayoongeza ukubwa wa tatizo hilo.

**UFUMBUZI**

Kuanzisha ofisi moja inayoshughulikia matatizo ya waathirika wa unyanyasaji iitwayo "One Stop Centre ianzishwe kwenye zahanati za vijijini, vituo vya afya vya kata na ofisi za serikali za mitaani kwenye majijini na miji.

Kadhalika kwenye hospitali za wilaya huduma hizo ziwepo, 'one stop centre' ziwe na daktari, polisi kushughulikia jinai, ustawi wa jamii na wanasaikolojia kutoa misaada ya kisheria na wanasheria kwa ajili ya kesi.

Lazima jamii iamke kuanzia viongozi wa dini, walimu, wazazi na wana familia kupinga ukatili wa kijinsi ili kila mmoja afahamu kubaka, ulawiti, ngono kinyume cha maumbile, kutelekeza, vipigo kuuana ni nini na ni hatia.

Kuwe na kufundisha maadili shuleni, kutoa elimu ya haki za binadamu na pia sheria nyingine kama ile ya kupima nasaba (DNA) na ile usafirishaji haramu wa binadamu zijulikane.

Wananchi wanatakiwa kufahamishwa kuwa kuna maabara zenye kipimo cha kupima DNA hivyo kuua, kukimbia mimba, kutelekeza familia siyo suluhu kuna hatua zaidi zinaweza kuchukuliwa na mtuhumiwa akaadhibiwa kisheria.

Ofisi ya ustawi wa jamii ya kijiji na polisi zipewe bajeti ili zipokee taarifa , kuzichunguza na kuzifuatilia na kuziwasilisha polisi wilayani na kwa Mkuu wa Wilaya mara moja kwa hatua.

UJIO BIDEN ANGOLA

# Mkakati wake reli ya madini DRC uboreshwe kujenga viwanda Afrika



Rais wa Marekani, Joe Biden na Rais wa Angola Joao Manuel Goncalves Lourenco (kushoto) katika Ikulu ya White House, Novemba mwaka jana. **PICHA: REUTERS**

**NA MWANDISHI WETU**

RAIS wa Marekani, anayemaliza muda wake, Joseph Biden, ameanza mwezi Desemba 2024 kwa kuitembelea Afrika.

Ni ziara inayomfikisha Angola taifa lenye utajiri mkubwa wa mafuta Kusini ya Jangwa Sahara, kufanikisha uwekezaji wa miundombinu ya reli itakayofanikisha kupata madini muhimu yanayohitajika duniani leo.

Safari ya Biden inalenga kushughulikia uwekezaji katika Ukanda au 'Corridor' ya Lobito, mradi wa reli ya maili 800 sawa na kilometa 1,600 unaounganisha Congo na Angola kusafirisha madini kutoka Congo kwenda Marekani na Ulaya, inasema televisheni ya Marekani ya CNN.

Ni uwekezaji unaoungwa mkono na Marekani na Umoja wa Ulaya (EU) ukilenga kusafirisha madini muhimu kutoka Afrika hadi bandari ya magharibi ya Angola ya Lobito kwa ajili ya kuyafikisha nchi za Magharibi, kwa mujibu wa CNN.

Mpango huo ni kitovu cha juhudi za utawala wa Biden za kuongeza uwekezaji barani Afrika ili kupunguzia kasi China kuwa na nguvu Afrika.

Inakumbusha kuwa China imemwaga mabilioni ya dola katika miradi ya miundombinu bara zima katika muongo mmoja uliopita.

Septemba mwaka huu, Rais wa China Xi Jinping wa China aliahidi msaada wa dola bilioni 50 kwa bara hilo na pia msaada wa masuala ya kijeshi.

Rais Biden pia atatembelea visiwa vya Cape Verde, akikutana na Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Ulisses Correia Silva.

Rais Biden anazuru bandari ya Lobito na kutembelea kiwanda cha kusindika chakula cha Carrinho, televisheni hiyo inaongeza.

Ukanda wa Lobito ni wa kwanza wa kimkakati wa kiuchumi unaosisiwa na Ushirikiano wa mataifa tajiri zaidi duniani G7 wa miundombinu na uwekezaji wa kimataifa (PGII) Mei 2023.

> "Waangola na Waafrika wanapokubali mradi huo ni aibu hawajisaidii wala Afrika. Kinachofanyika ni mwendelezo wa siasa za ukoloni mkongwe ulioanza miaka 1880 kwenye mkutano wa kuigawa Afrika."

Marekani na Umoja wa Ulaya (EU) zimeamua kuwekeza kwenye ukanda huo utakaofanikisha kuchimba madini hayo kutoka Congo na kuyapeleka kwenye viwanda vyao.

Mataifa yanayopitiwa na reli hiyo ni Angola, Congo DRC na Zambia pamoja na Tanzania kwa kuwa inatarajiwa kuendelea hadi kuwa na tawi kwenye Bahari ya Hindi.

**ANAIMALIZA AFRIKA**

Msomi na mchambuzi wa masuala ya maendeleo , ambaye ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha SAUTI Mwanza, Dk. Kamugisha Byabato, anapinga usafirishaji madini hayo.

"Waangola na Waafrika wanapokubali mradi huo ni aibu hawajisaidii wala Afrika. Kinachofanyika ni mwendelezo wa siasa za ukoloni mkongwe ulioanza miaka 1880 kwenye mkutano wa kuigawa Afrika."

"Kwanini msimamo usiwe Marekani na EU kuwekeza viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazotokana na madini hayo ya kimkakati? Bidhaa ni kama betrii za magari yanayotumia umeme, vifaa vya simu, ndege na bidhaa zote za kielektroniki?" anahoji Dk. Byabato.

Anashauri kijengwe kiwanda Angola au DRC na siyo kuchukua mali ghafi za Afrika leo baada ya miaka 150 ya mgawanyo wa Afrika uliofanyika Berlin Ujerumani.

"Afrika iamke sasa kuendeleza miundombinu ili kuboresha unyonyaji siyo suala jema. Kwa mfano Wajerumani walivyochukua makoloni Afrika, walipanga kujenga reli kutoka Namibia hadi Tanganyika kuunganisha himaya zao.

Tukumbuke baada ya kuigawa Afrika eneo lililo katikati ya Bahari ya Hindi na ya Atlantic liliitwa Congo Free Trade Area, ili kuruhusu liwe wazi kwa yeyote anayetaka kuvuna raslimali achukue ." anakumbusha mhadhiri huyo.

Anafurahia kujengwa reli hiyo na nyingine nyingi za kuunganisha nchi za Afrika, miji na miji na kanda kwa kanda kama ilivyo TAZARA akikumbusha kuwa ipo reli ya Trans Siberian Railways inayounganisha Ulaya Mashariki na Magharibi ikipita chini ya bahari hadi Urusi kwenye mji wa Vladivostok ambayo pia ni jirani na Japan.

Anaongeza kuwa kujenga reli ya Lobito DRC, Zambia hadi Tanzania ni jambo la kimkakati na bora zaidi kwa kuboresha mawasiliano kusini mwa Sahara na zinahitajika reli nyingi zaidi

"Itoke Dar es Salaam hadi Conacry Guinea, Cairo hadi Cape Town. Pamoja na barabara za kisasa na kuwepo mabasi ya kuzunguka miji mikuu ya Afrika nzima na si tena miundombinu ya kusafirisha raslimali za Afrika na kuiachia umaskini." Anaonya Byabato.

Kama zinavyoundwa ndege kuna kampuni zinatengeneza mabawa, injini, vipuri, vioo, mifumo ya umeme, ulinzi na umbo.

Lakini ni katika nchi mbalimbali pale kampuni husika ya kutengeneza ndege zinanunua vipuri na kuunganisha ili kupata ndege kamili, anaeleza.

Kuchukua kila kitu kutoka Afrika huku mataifa yakifurahia kana kwamba ni mafanikio wakati hatua hiyo ni sawa na ukoloni mkongwe na utandawazi unaoendeleza ubeberu, ni jambo la kukataa, anaongeza..

**TRUMP ATAKUBALI?**

Anapoulizwa iwapo mradi huo utafanikiwa kwa sababu Biden, anaondoka na Rais Donald Trump anachukua uongozi anajibu.

"Marekani ina sera ya mikakati ya kitaifa na kiongozi anayeingia ikulu haibatilishi. Kwa mfano wanasimamia na kulinda masuala makubwa ya kitaifa kama ulinzi, usalama, uwekzaji na biashara, kwa hiyo hata kama Rais Biden anaondoka mwezi ujao na Trump anachukua uongozi kama ni suala la kitaifa litaendelea.

SIKU 16 KUPINGA UKATILI

# Sumaiya Abadalla shujaa aliyeushinda mfumo dume

## •Mwanamke pekee dereva wa malori Z'bar

**NA RAHMA SULEIMAN**

NI wakati wa kupinga ukatili wa kijinsia na dhuluma wanazofanyiwa wanawake, wasichana na watoto na kukubali kwa matendo kuwa wote ni binadamu wana haki sawa bila kujali jinsi.

Ni kauli za wanaharakati mbalimbali wakati huu wa kuadhimisha siku16 za kupinga ukatili wa kijinsia, ambao unaakisi pia mafanikio tangu kufanyika mkutano wa dunia wa wanawake Beijing China mwaka 1995.

Jicho la harakati za juhudi za wanawake liko Zanzibar ambapo ni nadra kukutana na madereva wanawake wakiendesha magari makubwa ya mizigo, ingawa sheria hazikatazi.

Mwanamama Sumaiya Ali Abdallah, amevunja mwiko ni mwanamke pekee Zanzibar anayeendesha lori la mizigo kama ajira na chanzo cha kujipatia kipato.



Dereva Sumaiya akiwa kazini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Sumaiya (26) ni miongoni mwa wanawake 300 wa Zanzibar wenye leseni ya udereva lakini ni yeye pekee mwenye leseni ya daraja la C inayotumiwa na madereva wa magari makubwa ya mizigo.

Takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, zinasema wapo madereva 10,717 kwa mwaka jana kati ya hao asilimia chini ya 10 wanawake.

Akiwa mtoto wa kwanza katika familia ya watoto sita Sumaiya, anaendesha lori linalobeba makontena kituo chake cha kazi ni bandarini Malindi Unguja, akitoa shehena bandarini kuzipeleka ndani na nje ya Zanzibar.

Anapozungumza na Nipashe, anasema ni ndoto yake kuendesha magari makubwa baada ya kuona kazi hiyo ikifanywa zaidi na wanaume wakati si haramu mwanamke kuendesha lori.

"Kabla sijaanza kazi hii nilikuwa natamani siku moja niendeshe magari makubwa ya kubeba mizigo, maana barabarani nilipowaona wanaume wakiendesha huwatazama na kujiuliza hivi siwezi kuendesha gari kama lile? Nashukuru kuwa hivi sasa maswali yangu yamejibiwa na kutimiza ndoto zangu", anasema.

Dereva huyo anasema hajaolewa, akisimulia kuwa kazi hiyo ya kuendesha lori la mizigo bandarini amedumu nayo kwa miaka mitatu sasa na mwanzo alianza kuendesha gari la tani nne la kubeba mchanga na sasa anaendesha lori la tani 10.

"Mwanzo nilianza kubeba mchanga eneo la Donge Kaskazini Unguja nikipeleka maeneo mbalimbali kisiwani hapa", anasema.

**FIKIRA MFUMO DUME**

Sumaiya wakati anaanza kazi wapo baadhi ya watu walimshangaa lakini wengine wakampongeza kwa ujasiri.

"Walionishangaa walitawaliwa na mfumo dume wakiamini kuwa kazi hiyo ni ya wanaume. Kwa sasa jamii inaniunga mkono kutokana na uamuzi wangu huo na wakati mwingine ninapokuwa barabarani nikishikilia usukani napokea pongezi nyingi."

Anasema anapigiwa honi na madereva wengine na anaamini kuwa zinaashiria pongezi kwa jukumu hilo.

Anasimulia kuwa kuna wakati akiwa barabarani anakutana na watoto wa kike na wakiume wamejipanga wakimpigia makofi na kumpongeza hasa nyakati za kurudi nyumbani akitokea shuleni.

Sumaiya anasema kufanya kazi hiyo ya udereva hakumzuwii kuendelea na majukumu mengine ya kifamilia mfano usafi wa nyumba, kupika na kushiriki katika harakati za kijamii.

Anasema kabla ya kusomea udereva alijifunza uandishi wa habari akiwa na stashahada na kuifanyia kazi kwa muda mfupi lakini ilimshinda kwa sababu aliona hajatimiza ndoto yake.

**RUSHWA YA NGONO**

Sumaiya anazungumzia vitendo vya rushwa ya ngono katika kazi hiyo, akisema hajakumbana navyo, akisema kama dereva anajiheshimu na anaheshimika wenzake kazini.

"Mimi sijaolewa wapo ambao wananifuata kwa ajili ya kuanzisha mahusiano lakini haina maana kuwa labda ni ving'ang'anizi kutaka rushwa ya ngono hapana, unapowaambia ukweli kwamba sipo tayari na hilo wanakuelewa," anasema.

Changamoto, anayokutana nayo Sumaiya ni baadhi ya madereva hasa wa bodaboda hawafuati sheria za barabarani na kuongeza usumbufu.

**UJUMBE KINAMAMA**

"Tuache kuchagua kazi kwa visingizio vya mitazamo hasi ya kwamba kazi ngumu ni za wanaume pekee. Hakuna aliyejua kuwa Tanzania itaongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwanamama leo imewezekana."



Sumaiya anaishauri Serikali ya Zanzibar kuongeza vyuo vya ufundi wa udereva wa magari makubwa ya kusafirisha shehena kama ilivyo kwa nchi nyingine pamoja na Tanzania Bara ili ndoto za vijana wengi wa kike na kiume kutimia.

"Udereva nilianza kujifunza hapa Zanzibar lakini wa malori ya shehena nilijifunza chuo cha ufundi VETA Tanzania Bara kwa sababu Zanzibar hakuna kozi hiyo," anaeleza.

**WANAFAMILIA**

Baba wa dereva huyo Ali Abdallah anasema amefurahi kumuona binti yake amechagua kazi anayoipenda mwenyewe ambayo inamwingizia kipato.

"Huu ni uamuzi wake na sisi familia yake na wazee wake kwa ujumla tumeridhia na kumpa baraka zote binti yetu ni kazi kama nyingine," anasema.

Aidha, ni vyema kuwaunga mkono watoto wenye vipaji kwa kuwaendeleza ili kujipatia kipato halali ambacho kitasadia kuongoza familia zao, anasema.

Wanaharakati wa haki za wanawake, wanasema kwa miaka mingi watoto wa kike wamebaguliwa katika harakati za maendeleo kutokana na mifumo dume iliyojengeka katika jamii.

Dk. Mzuri Issa Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar anasema mtoto wa kike anachukuliwa kama mtu wa kulea familia na hastahiki kufanya kazi ya kumuingizia kipato.

"Ndiyo maana uchumi wa wanawake ni mdogo ikilinganishwa na wanaume kwa sababu tangu zamani mwanamke hakujengwa kuwa kiongozi bali kuwa mama wa kulea familia", anasema Dk. Mzuri.

Kadhalika anasema wakati umefika kwa watu wa jinsi zote kushiriki katika kila harakati za kimaendeleo, kiuchimi kisiasa na kijamii bila ya vikwazo.

Sajenti Ali Abdallah, kutoka Ofisi ya Usalama Barabarani Polisi Makao Makuu, Zanzibar, anasema madereva wanawake ni mahiri zaidi katika kufuata sheria za barabarani wanapoendesha vyombo vya moto kuliko madereva wanaume.

Anasema katika ajali zinazotokea barabarani nyingi husababishwa na madereva wanaume kwa sababu mbalimbali ikiwemo uzembe wa madereva hao na kutofuata sheria za usalama.

"Madereva wanawake ni makini zaidi wakati wanapoendesha gari na si rahisi kumkuta na makosa ya usalama barabarani, laiti nchi hii ingekuwa na madereva wanawake watupu ajali za barabarani zingekuwa chache mno," anasema Sajenti Ali.

Sheria za Zanzibar hazikumnyima fursa ya mwanamke kuendesha gari kama ilivyo kwa baadhi ya nchi mfano Oman ambayo nayo sasa imeondoa zuio hilo.

Chama cha madereva wa malori Kenya kinaeleza kuwa kuna wanawake 100 wanaoendesha malori.



## Serikali kujenga uwezo wa kufanya tathmini za miradi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali Ofisi ya Waziri Mkuu, Sakina Mwinyimkuu amesema serikali imedhamiria kujenga uwezo wa kufanya tathmini za programu na miradi kwa vitendo kwa kutumia mifumo halisi inayotekelezwa nchini.

Alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku nne ya kuwajengea uwezo wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini kujifunza kwa vitendo.

Alisema katika kutekeleza hilo, mafunzo maalum kwa wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini yameanza kutolewa, ambapo washiriki watapata fursa ya kujifunza namna ya kufanya tathmini za programu ambapo kwa kuanzia washiriki watatumia Programu ya Uendelezaji wa Kilimo nchini (ASDPII).

"Programu hii inalenga kuboresha sekta ya kilimo kwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuboresha maisha ya mkulima na kuwa na kilimo endelevu nchini," alisema Sakina.

Aliongeza kuwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya II ni programu ya kimkakati inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu- Sera, Bunge na Uratibu.

"Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Tathmini ya Ujerumani (DEval) na Kituo cha Kujifunza Tathmini na Matokeo cha Afrika ya Kusini ((CLEAR - AA) wameandaa warsha ya kujengea taasisi za umma katika kufanya tathmini za miradi na programu mbalimbali," alisema Sakina.

Aidha, alisema kuwa utekelezaji wa programu hiyo unaonyesha juhudi za serikali katika kuongeza kipato cha mkulima na kuwezesha ukuaji wa uchumi wa taifa.

Alisema: "Mafunzo haya ni mwanzo wa mafunzo ya vitendo yatakayoendelea kutolewa kwa watumishi wa umma na kujifunza namna ya kufanya tathmini za miradi na programu kwa vitendo".

# Wanandoa wapewa mbinu kuepuka maambukizi VVU

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe amewataka wanandoa kuwa waaminifu ili kupunguza migogoro na magonjwa mbalimbali, ikiwamo maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Alisema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika ukumbi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida.

Gondwe ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego katika maadhimisho hayo aliwahimiza wakazi wa Singida kuwa waaminifu katika uhusiano ili kuepusha mambo mengi ya magonjwa, kwani kufanya hivyo kunaweza kuepusha ugomvi katika ndoa pamoja na maambukizi ya VVU.

"Mnatakiwa muwe waaminifu katika ndoa na wote waliokaribia kuoa, hii itaepusha vitu vingi ikiwemo migogoro ya ndoa pamoja na magonjwa," alisema.

Gondwe aliwataka wanafunzi kuacha tamaa ya kutamani vidogo vidogo ambavyo vinasababisha wanaingia katika mahusiano yasiyo salama na kusababisha kupata maambukizi ya VVU.

Aidha, aliwataka wananchi kuwapenda na kuwajali wale ambao wamepata VVU wasiwatenge.

"Wanandoa wawe waaminifu kwa wenza wao, pia ni vema kuwapenda, kuwajali na kuwahudumia waathirika wa VVU, pia ni vema vijana wakaacha tamaa za maisha mazuri ili kuepuka vishawishi ambavyo vinasababisha kujiingizia katika vitendo vinavyoweza kusababisha kupata maambukizi ya VVU," alisema.

Meneja mradi kutoka USAID, Said Mgeleka alisema kwasasa dawa za kufubaza VVU zinapatikana kwa urahisi na kwa wingi tofauti na miaka ya nyuma, kwamba iliwalazimu watu wa makundi maalum pekee kama wamama wajawazito wakati wa kujifungua pekee.

Alisema: "Kwasasa dawa za ARV zinapatikana katika ngazi zote siyo tu katika hospitali za mikoa na taifa bali mpaka katika zahanati zote vijijini kwani tangu mwaka 2016 juhudi za serikali na wadau zimewezesha utoaji wa dawa hizo kwa yeyote yule atakayegundulika na maambukizi bila kujali wingi wa CD4 au dalili yeyote ya magonjwa nyemelezi".



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego (kushoto), akizungumza na mkazi wa kijiji cha Kinku, wilayani Ikungi, Beritha Dulle ambaye nyumba yake imebomoka na kuezuliwa paa kutokana na mvua kubwa ya mawe iliyoambatana na upepo mkali iliyonyesha, kijijini hapo juzi na kusababisha kaya zaidi ya 24 kukosa makazi, alipotembelea eneo hilo, jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TBS: Wazalishaji bidhaa za zabibu thibitisheni ubora

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wazalishaji wa bidhaa zitokanazo na zabibu kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ili kuwa na uhakika wa soko ndani na nje ya nchi.

Rai hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na maofisa wa TBS kwenye maonesho ya kimataifa ya wawekezaji katika zao la zabibu Dodoma, yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mashujaa jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa TBS kwenye maonesho hayo, mmoja wa maofisa hao Domisiano Rutahala alisema maonesho hayo yamekuwa fursa muhimu kwa shirika hilo.

Alisema kupitia maonesho hayo wametoa elimu kwa wazalishaji hasa wajasiriamali kuhusiana na faida za kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ili ziweze kutumia alama ya ubora ya TBS.

Alisema kupitia maonesho hayo yenye kauli mbiu isemayo; "Zabibu fursa ya uwekezaji na chachu ya maendeleo nchini" wametoa elimu kuhusiana na utaratibu wa kufuata ili kupata nembo ya ubora, kwani TBS ni taasisi rafiki ambayo ipo karibu sana na wajasiriamali, ambapo serikali inatenga fedha kwa ajili ya kuwahudumia bure.

"Kwa hiyo serikali kupitia TBS inatoa huduma hiyo ya kuthibitisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali pasipo kulipia gharama zozote," alisema

Alifafanua kwamba Mkoa wa Dodoma ndiyo eneo pekee nchini linalozalisha zabibu na wazalishaji wengi wa bidhaa zitokanazo na zao hilo wapo Dodoma hususani wajasiriamali, hivyo baada ya maonesho haya kupitia elimu tuliyowapatia, wengi watakuja kuthibitisha bidhaa zao.

Alisema wanachotakiwa kuwa nacho ili kuweza kuthibitishiwa ubora bidhaa zao na TBS bureni barua ya utambulisho kutoka SIDO na baada ya hapo mchakato unaanza.

Kadhalika, alisema wakishapata nembo ya ubora, itawasaidia kuuza bidhaa zao katika masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi, hivyo hawatakuwa wasindikizaji kwenye soko.

Alitoa mfano akisema nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimeingia makubakubaliano ambapo bidhaa ikishathibitishwa ubora na shirika la viwango la nchi husika ikienda nchi nyingine haitakiwi kupimwa tena.

Rutahala alisema hiyo ni fursa muhimu kwa wajasiriamali kuweza kufikia masoko ya nje ya nchi.

"Kwa hiyo msisitizo wetu kwa wazalishaji, hasa wajasiriamali wasizalishe bidhaa ambazo ambazo hazijathibitishwa ubora na TBS vinginevyo watashindwa kufikia masoko ya kikanda na kimataifa.

Alisema: "Hatutaki wazalishaji hasa wajasiriamali wawe wasindikizaji kwenye soko kwa kuzalisha bidhaa ambazo hazina viwango, ndiyo maana serikali inatenga fedha nyingi kwa ajili ya kuthibitisha bidhaa zao".



# Mbeya yaanza mapambano kutokomeza ajali barabarani

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Polisi kwa kushirikiana na Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya limezindua wiki ya nenda kwa usalama ndani ya mkoa huo.

Lengo ni kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika kipindi cha mwisho wa mwaka.

Kampeni hiyo ilizinduliwa katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mkoa wa Mbeya ambapo maofisa mbalimbali wa jeshi hilo na baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walitoa elimu kwa madereva na kwa abiria kuhusu namna ya kuepuka ajali.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Polisi, Notika Kiwale, aliwataka abiria wanaopanda kwenye magari ya abiria kutoa taarifa kwenye mamlaka wanapoona mwenendo wa dereva hauwaridhishi.

Alisema dereva yeyote ambaye atakamatwa akikiuka sheria za usalama barabarani, atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani ambako anaweza akafungwa kifungo cha miezi sita, kufungiwa leseni yake ama vyote viwili.

Hivyo, aliwataka madereva kuhakikisha wanafuata sheria za usalama barabarani, ili kuepuka adhabu hizo ambazo zinaweza zikaharibu mwelekeo wa maisha yao.

Alisema wapo baadhi ya madereva ambao wamekuwa wakikiuka sheria kwa kulazimisha kuyapita magari mengine hasa kwenye maeneo ya miinuko na kwenye kona.

"Kazi yenu abiria ni kutoa taarifa kuhusu dereva anayekiuka taratibu barabarani, toa taarifa kwa mtu yeyote ambaye unaamini kwamba anaweza akasaidia hatua zikachukuliwa haraka na kuokoa maisha yenu," alisema Kiwale.

Alisema waliamua kuzindua kampeni hiyo mwishoni mwa mwaka kwa sababu ni kipindi ambacho ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kusababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

Kaimu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hope Maliki, aliwataka madereva kuhakikisha wanaendesha magari kwa kuzingatia alama za usalama barabarani ili kuwafikisha abiria salama kwenye maeneo wanayoenda.

Alisema kwa magari ambayo yanasafiri umbali wa zaidi ya kilomita 500 ni lazima yawe na madereva wawili ambao watakuwa wanapokezana kuendesha ili kuepuka uchovu kuwa chanzo cha ajali.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu (kushoto), akipokea mbegu ya mti kutoka kwa Shekhe wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Njalambaha, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji wa miti, jijini Mbeya juzi, iliyoanzishwa na Mufti wa Tanzania, kwa ajili ya nchi nzima. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TBS: Watanzania someni taarifa zilizoandikwa kwenye bidhaa

**Na Nebart Msokwa,**
SONGWE

WATANZANIA wamehimizwa kujenga utamaduni wa kusoma taarifa zilizoko kwenye vifungashio vya bidhaa wanazotaka kununua.

Lengo ni kujiridhisha kama ni salama kwa matumizi ya binadamu ikiwa ni pamoja na kujua muda wa matumizi.

Ofisa Masoko wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mussa Luhombero aliyasema hayo wakati wa kampeni maalumu ya elimu kwa umma inayotolewa na shirika hilo kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa zenye ubora.

Elimu hiyo ilitolewa kwa wananchi kwenye Halmashauri ya Wiilaya ya Mbozi, Songwe, Momba na Tunduma mkoani Songwe ambao ni miongoni mwa mikoa yenye mwingiliano mkubwa wa bidhaa kutoka mataifa jirani.

Alifananua kuwa TBS imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya viwango katika ngazi za wilaya nchini ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu bidhaa wanazonunua.

"Wito wetu kama shirika ni kuhimiza wananchi mnaponunua bidhaa mkumbuke kusoma taarifa zilizopo kwenye vifungashio, ambazo zitawapa uhakika kuwa zimethibitishwa ubora na TBS, bidhaa hizi zisipokuwa na ubora zinaweza zikawa hatari," alisema Luhombero.

Alisema endapo wananchi watakuwa na utamaduni wa kusoma taarifa za bidhaa hizo, wataepuka kutumia bidhaa ambazo zimekwisha muda wa matumizi na hivyo kuwa salama kiafya.

Pia, alisema kupitia kampeni hiyo wanahamasisha wajasiriamali wadogo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao na wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi ili wawe na uhalali wa kuuza bidhaa hizo.

Alisema kampeni hiyo inafanyika katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya sokoni, vituo vya mabasi, minadani na maeneo mengine ya wazi ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Luhombero aliwataka wajasiriamali na wafanyabiashara kuhakikisha wanauza bidhaa zilizothibitishwa ubora na TBS na wenye majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi kuyasajili ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

## Wataja chanzo viuatilifu kushindwa kufanya kazi shambani

**Na Mwandishi Wetu**

WATAFITI na wadau wa kilimo wamesema kutokuwa na uelewa kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo kunasababisha matumizi ya viuatilifu vitokanavyo na viumbe hai kudhibiti visumbufu vya mazao kuwa madogo kwa wakulima nchini.

Hayo yameelezwa juzi katika mkutano uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) uliowakutanisha watafiti na wadau mbalimbali wa kilimo kujadili namna ya kuongeza matumizi ya viuatilifu vitokanavyo na viumbe hai na kupunguza matumizi ya pembejeo zenye kemikali.

Pia, ulilenga kudhibiti visumbufu vyenye madhara kwa mazao, ardhi na watumiaji wa mazao.

Mtafiti wa mradi wa Agro-biological, Dk. Mesiah Ilomo alisema matumizi ya pembejeo zitokanazo na viumbe hai yamekuwa ni madogo nchini kutokana na baadhi ya changamoto walizoziainisha, ikiwamo kuwa na uelewa mdogo juu ya viuatilifu hivyo na gharama kuwa juu.

Dk. Ilomo ambaye ni mhadhiri wa UDSM alisem mwamko mdogo wa wakulima juu ya matumizi ya viuatilifu vitokanavyo na viumbe hai ni sababu kuu ya kuitisha mkutano huo.

Alisema mkutano huo umelenga kukutanisha wadau ambao ni watafiti, watunga sera, wasimamizi wa serikali, wamiliki wa kampuni za pembejeo na wadau mbalimbali ili kujadili kuhusu pembejeo hizo.

Mtafiti wa viuatilifu kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), Ramadhani Kilewa alisema viuatilifu vingi vinaagizwa kutoka nje.

Alisema lakini sasa mwamko umeanza kuingia nchini na kuna baadhi ya viwanda ambavyo vimeanzishwa kwa ajili ya kutengeneza viuatilifu vitokanavyo na viumbe hai.

"Wengi wanaamini viuatilifu vinavyotokana na viumbe hai viko salama lakini Sheria ya Afya Namba 104 ya Mwaka 2020 imeweka utaratibu wa namna ya kutengeneza, kuagiza kufanya usajili, kusambaza na kuuzwa ili kuhakikisha viuatilifu vinavyotumiwa na wakulima kudhibiti visumbufu vinakuwa na ubora na salama kwa afya ya binadamu," alisema.

Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Idara ya Sayansi ya Mazao na Mazao ya Bustani, Ramadhani Majubwa, alisema wanafanya utafiti ni kwa namna gani teknolojia za kilimo hai zinafanya kazi.



# Serikali: Mkataba wa ILO umeanza kujadiliwa SMT, SMZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif amesema mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), umeanza kujadiliwa katika ngazi ya wataalamu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Muhammed Ali Suleiman aliyetaka kujua, ikiwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni sababu gani za msingi zilizoifanya kushindwa kuuridhia mkataba wa kimataifa Na. C190.

Mkataba huo unalenga kupinga ukatili wa kijinsia mahali pa kazi, ukiwa ni mkataba jumuishi unaohusisha wafanyakazi wote, sekta rasmi au zisizo rasmi.

Akijibu swali hilo, Shariff alisema ofisi imekuwa ikipokea malalamiko na migogoro ya kazi kwa maeneo mbalimbali ya kazi katika masuala ya haki za mikataba, mishahara, kufukuzwa kinyume na taratibu, udhalilishaji wa kijinsia.

Aidha, alisema Sheria ya Kazi, Sheria ya Ajira Namba 11 ya Mwaka 2005, Kifungu cha 10 kinakataza ubaguzi wa aina yeyote katika kazi.

"Kifungu hicho kinahimiza fursa sawa, malipo sawa, bila ubaguzi wa kutofautisha, kupendelea, kutenganisha. Kifungu cha 11 kinakataza unyanyasaji wa kijinsia katika ajira (ngono - ama waziwazi au sio wazi, lugha chafu, vitisho, ahadi za ngono, tabia za uasharati)". Alisema.

Aidha, alisema uwepo wa kanuni ya kuzuia na kupinga unyanyasaji wa kijinsia ambapo suala la unyanyasaji wa kijinsia lina sura mbili kisheria ukiwamo wa jinai.

# Dk. Mwinyi atoa agizo kuhusu mitaro ya Mji Mkongwe

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiagiza Mamlaka ya Mji Mkongwe kufunika mitaro (mifereji) kwenye mji huo, ili kuepusha maradhi na ajali kwa wananchi na wageni wanaoutembelea mji huo.

Alitoa agizo hilo wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mji Mkongwe wa Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Bustani ya Forodhani, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema kuwa kuwepo wazi kwa mitaro hiyo hakutoi haiba na taswira njema ya Mji Mkongwe na kushusha hadhi ya kuwa mji wa urithi wa dunia unaotambulika na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni tisa kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa majengo yaliyo katika hali mbaya zaidi ndani ya Mji Mkongwe ambayo wananchi hawamudu gharama za kukarabati.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali ipo katika hatua za kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kupitisha chini ya ardhi miundombinu yote ya umeme, mawasiliano na maji katika Mji Mkongwe ili kurejesha haiba ya taswira ya majengo hayo kupitia mradi wa BIG Z wa Benki ya Dunia (WB).

Alisema Mji Mkonge hautoweza kubaki hai endapo hautofanyiwa matengenezo makubwa yanayohitaji nguvu ya kila mmoja ikiwamo wananchi wa mji huo, taasisi za umma na binafsi kwa kuhakikisha kila mmoja anatoa mchango wake katika kuutunza, kuuhifadhi na kuuendeleza mji huo.

Hivyo, aliwahakikishia wakazi wa Mji Mkongwe kuwa serikali itaendelea kushirikiana na wadau, taasisi za ndani na kimataifa ili kuhakikisha Mji Mkongwe unaimarika na kubaki kuwa kioo cha maendeleo na utalii wa Zanzibar kwa maslahi ya vizazi vya sasa na baadaye.

Aliishukuru Serikali ya Oman kwa kuunga mkono juhudi za Zanzibar za kuuhifadhi Mji Mkongwe na maeneo mengine ya kihistoria yaliopo Zanzibar, akisema msaada huo umechangia kuyaweka maeneo hayo kuwa endelevu wakati wote.

Kadhalika, aliitaka Serikali ya Oman kuendelea kuwajengea uwezo watendaji na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ikiwamo ujuzi ambao umewaongezea weledi wanaoutumia katika kuendeleza mji huo.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudriki Ramadhan Soraga, alisema mabadiliko chanya uongozi wa serikali yameleta mabadiliko makubwa kwa Mji Mkongwe na kuuongezea umaarufu zaidi kimataifa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, Ali Said Bakari, aliishukuru Serikali ya Oman kwa msaada wa Dola za Marekani milioni 25 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Beit el Ajaab.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yawatambua 'Makachu' kivutio utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imesema kuwa vijana wanaopiga mbizi baharini katika eneo la Forodhani maarufu 'Makachu' ni kivutio kikubwa cha utalii.

Amesema vijana hao wamekuwa wakionyesha ustadi wao wa kupiga mbizi mbele ya wageni wanaotembelea Zanzibar.

Alisema hayo juzi katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir.

Ameir alitaka kujua kwa kiasi gani vijana wanaopiga mbizi maarufu kama makachu waliopo Forodhani, wanaendelea kuitangaza vyema Zanzibar kupitia sekta ya utalii, kupitia mitandao ya kijamii, video na picha za vijana hao zimeenea sehemu mbalimbali na kulitangaza jina la Zanzibar kimataifa.

Akijibu swali hilo, Soraga alisema mtindo huo wa kipekee wa sanaa ya mbizi siyo tu unatoa burudani bali pia unawavutia watalii na kuchangia katika kutangaza utamaduni wa Zanzibar kimataifa.

"Vijana wa "makachu" wamevutia wageni mashuhuri wengi, wakiwamo watu maarufu duniani kutoka kwenye sekta za burudani, siasa na michezo," alisema.

Soraga aliwataja baadhi ya wageni hao mashuhuri ambao wamevutiwa na sanaa na mchezo huo ni pamoja na wasanii wa kimataifa, wanamitindo, viongozi wa kitaifa na kimataifa ambao wameweka nia ya kutembelea Zanzibar kwa lengo la kuona ustadi wa vijana hao.

Alisema wizara yake kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe inawatambua vijana hao rasmi na imeshafanya uchaguzi wa uongozi wa kikundi hicho.

Alisema Mamlaka ya Mji Mkongwe inaimarisha usalama wa wapiga makachu hao kwa kuweka mstari maalum katika ukuta wa Forodhani ili kuweza kujua kina cha maji kilicho salama kwa kuogelea.

Waziri Soraga alisema mamlaka hiyo imetoa mwongozo kwa vijana hao katika kuimarisha usafi wa eneo hilo pamoja na kulinda mila na silka za Wazanzibari.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**VAILETH PHONETA MNDEME** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0308-0084** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ENABOISHU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016, Cheti hiki kimepotea Jijini DODOMA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/50893/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LYNETH TETA LUCAS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0249/0064** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LORETO GIRLS' SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/265102/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FAIDA MARCO DALUSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2086/0042** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KAKORA SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KMR/RB/5960/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASAJILE CLINTON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **P1377/0218/2017** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NATIONAL CORRESPONDENCE INSTITUTE CENTRE** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/ILA/264925/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NDG. SHAFII SHOMARI NILONGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **Bajaji boxer** yenye namba za usajili **MC 967 DTQ ,** Engine namba **JUXWNJ47919,** Chassis Namba **MD2BL5BX6NWJ97137** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA **POLISI:PHQ/NJO/NJO/5856/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KARIM HASSAN MKOREHE**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T721 BVB ILIYOPOTEA. HIVYO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE. POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/MUF/16719/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISACK HANCE SENTI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 983 EBP** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MBE/RUN/39720/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MEDAN SAMSON CHAMHA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 667 DZV** ,iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/KIN/266947/2024.**

## KADI ZA GARI ZIMEPOTEA

Ndugu **FURAHA NAZARETH MWAMBONA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye usajili ; **T.491 DUR.** Yenye Chasis namba **P193016,** Engine namba: **U819049.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **PHQ/ARU/ARU/46427/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 29088 of 2024**

**In the matter of the estate of the late MARY MBEZI MHINA of ITEGA within Dodoma City**

**And**

**In the matter of an application for letters of administration by ELIZABETH GEORGE MBEZI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 day of 12............................2024

Dated at Dodoma this 3 Day of 12 ................2024.

...................
RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 66174/2024**

**FATUMA SELEMANI BILALI ..............................MLETA RUFAA**

**DHIDI YA**

**MOSES JACKSON MAKAPI....................................MJIBU RUFA**
**GAUDENCIA SAMSON MTATIRO.........................MJIBU RUFAA**
**MWAJUMA SALUM KARABAKI.............................MJIBU RUFAA**
**EMMANUEL ANANIA.......................................MJIBU RUFAA**
**MARIAM KINABO................................................ MJIBU RUFAA**

**KWA: MOSES JACKSON MAKAPI**
**GAUDENCIA SAMSON MTATIRO**
**MWAJUMA SALUM KARABAKI**
**EMMANUEL ANANIA**
**MARIAM KINABO**

**POPOTE PALE WALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA.66174/2024**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma, mbele ya **MHE. JAJI I. D. MUSOKWA** , wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma , saa tatu kamili (9:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 10/12/2024.

HIVYO BASI; Mnatakiwa Mfike wenyewe au mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .

**NA ENDAPO;** Hamtofika wenyewe au mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakanyoamua pasipo nyie au mawakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 12 mwezi wa Novemba,2024.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki na wakurugenzi wa kampuni ya
**GLOBE TRADE LIMITED**
yenye namba za usajili **169429405,** wanapenda kuutangazia umma kuwa kutokana na kushindwa kujiendesha, wamiliki wameamua kuifunga kampuni kwa mujibu wa sheria za **BRELA.**
Hivyo tunaomba kama kuna mtu yoyote ana pingamizi, malalamiko au madai yoyote awasiliane kwa njia zifuatazo.
**Email:**
**globetradeltd2023@gmail.com.**
**Simu: 0785 110 786**

**AKIL ALIRAZA GULAMHUSSEIN**
**MKURUGENZI MTENDAJI**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29998 OF 2024**

**IN the Matter of the late: JOSEPH GERALD MKUDE**

**1. ROSE CHRISTOPHER LUKOSI**
**2............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 5th day of AUGUST, 2024.
Dated at Morogoro this **26TH day of NOVEMBER 2024**

...................
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 29089 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE OF THE LATE FRIMATH PAUL MASSAWE OF MKALAMA STREET WITHIN DODOMA REGION.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**BESSY WALTER MAIMU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 10 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 31 Day of January, 2025
Dated at Dodoma this 29 Day of 11, 2024.

...................
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**

**MOROGORO SUB REGISTRY**
**AT MOROGORO**

**LAND APPEAL NO. 25154 OF 2023**

**(Originating from Applicant No.63/2019 of the Kilombero/Malinyi District Land and Housing Tribunal)**

**BETWEEN**

**MATELINI DAMIANI MANYINYI..........................APPELANT**

**VERSUS**

**MAIKO MAULID.............................................RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: MAIKO MAULID............RESPONDENT**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention on 10th day of DECEMBER 2024 at 09:00 A.M before **Hon. H. KINYAKA, J.** at the High Court of Tanzania at Morogoro.
Your required to appear in person or through your Advocate or agents dully authorized to appear on your behalf.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed with the appeal for hearing in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 25th day of November, 2024.

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi**
**Kwa Bei Poa**
**Tupigie: +255 - 0677 020701**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# DRC yaiburuza Rwanda Mahakama ya Afrika

**KINSHASA, DRC**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imesema inaendelea na kesi dhidi ya Rwanda mbele ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Kibinadamu na Watu, kwa lengo la kudai haki dhidi ya mauaji na uporaji yaliyofanyika DRC, kwa madai kwamba yalitekelezwa na waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa Sheria wa DRC, Samuel Mbemba, akieleza kuwa kesi hiyo itasikilizwa Februari 12, 2025, katika mahakama hiyo iliyo chini ya Umoja wa Afrika (AU) yenye makao yake makuu jijini Arusha.

Ilielezwa kuwa kesi hiyo ni sehemu ya mfululizo wa mipango ya kimataifa ya kisheria inayolenga kuangazia ukiukaji unaofanywa na Rwanda na rais wake, Paul Kagame, katika ardhi ya Congo.

"Kwa miongo kadhaa ya uchokozi dhidi ya nchi yetu, uporaji wa madini yetu, ubakaji wa watoto wetu na wanawake wetu, na mauaji ya watu wetu, Rwanda na Paul Kagame hawajawahi kufunguliwa mashtaka kwa kesi za kweli," alisema Mbemba.

Pia ilielezwa kuwa tofauti na kesi iliyosikilizwa Septemba 26, mwaka huu mbele ya Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), iliyohusu migogoro mahususi ya kikanda, kesi hiyo mpya ni sehemu ya mchakato mpana zaidi.

Waziri huyo anayeshughulikia mizozo ya kimataifa alisema kesi hiyo inalenga kuwajibika kwa miongo kadhaa ya uchokozi, uporaji wa maliasili, unyanyasaji wa kingono, na mauaji yanayowakabili wakazi wa Congo.

"Huu sio ukosoaji wa kawaida ambao tulizoea. Kuna kesi tatu ambazo zinaendelea leo 'jana'," alisema .

Ilielezwa kuwa kesi hiyo inaonyesha nia ya wazi ya DRC ya kuhamasisha mamlaka za kimataifa kukomesha hali ya kutokujali ambayo kwa kawaida Rwanda inanufaika katika mazingira ya migogoro ya Mashariki. Hata hivyo, ilielezwa kuwa kwa kutegemea mamlaka ya Umoja wa Afrika, mchakato huo unatafuta kufungua njia mpya ya utambuzi wa haki za watu walioathirika na kuelekea katika taasisi nyingine kama mahakama ya kimataifa ya uhalifu.

**RFI**

## Afrika Kusini yatwaa uongozi G20

**PRETORIA, Afrika Kusini**

AFRIKA Kusini imekuwa nchi ya kwanza barani Afrika kuongoza kundi la mataifa yenye nguvu, maarufu kama G20, huku Rais Cyril Ramaphosa akiielezea nafasi hiyo kama muhimu kwa taifa hilo.

Akizungumza na wandishi wa habari jana katika jimbo la Limpopo, Rais Ramaphosa alisema taifa hilo lilitwaa rasmi uongozi huo juzi, akisema licha ya uchumi wa nchi yake kuwa mdogo, lakini wamefanikiwa kuwa sehemu ya G20

Alisema nchi za G20 zinachangia takribani asilimia 75 za biashara ulimwenguni jambo ambalo ni fursa nzuri kwa Afrika Kusini.

Rais Ramaphosa pia aliahidi kufanya kazi kwa ukaribu na Rais mteule wa Marekani Donald Trump, akigusia kuwa Marekani itakuwa Rais wa G20, ifikapo 2026.

Awali, kiongozi huyo alisema kuwa atatumia nafasi ya uongozi wa Afrika Kusini ndani ya G20 katika kukuza ukuaji wa uchumi jumuishi na maendeleo endelevu, na kwamba Pretoria imepitisha mshikamano, usawa na uendelevu kama dhima yake wakati ikishika hatamu ya G20.

Kwa mujibu wa Ramaphosa, Afrika Kusini itaendelea kuimarisha na kuendeleza harakati za pamoja za Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

"Iwe ni Gaza, Sudan, au Ukraine, lazima sote tusimame katika mshikamano na watu hao ambao wanakabiliwa na shida na mateso," Ramaphosa alisema, akiongeza kuwa ni lazima kwa G20 kuunga mkono nchi zilizo hatarini.

**TRT**



Rais wa Marekani Joe Biden akiwasili Angola, jana. **PICHA: MTANDAO.**

# Biden atembelea Angola kwa mara ya kwanza

**LAUNDA, Angola**

RAIS wa Marekani Joe Biden ametembelea Angola kwa ziara yake ya siku tatu iliyosubiriwa kwa muda mrefu na mataifa ya kusini mwa Jangwa la Sahara.

Ilielezwa kuwa Rais Biden aliwasili nchini humo na kulakiwa na maelfu ya raia wa Angola na katika ziara hiyo atajikita katika mradi mkubwa wa reli unaoungwa mkono na Marekani ulio na lengo la kukabiliana na ushawishi wa China katika bara la Afrika.

Mradi huo wa reli wa Lobito Corridor utakaoshuhudia kuimarishwa kwa reli inayopitia Zambia, Congo na Angola unalenga kuendeleza uwepo wa Marekani katika eneo hilo lililo na madini muhimu yanayotumika katika betri za magari ya umeme, vifaa vya kielektroniki na nishati safi ya teknolojia.

Ilielezwa kuwa ziara hii ya Biden inakuja wiki chache kabla ya Rais mteule Donald Trump kuchukua mamlaka rasmi Januari 20, mwakani, na kwamba ziara safari hiyo inatimiza ahadi yake ya kuzuru nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara.

Biden atasafiri katika mji wa bandari wa Lobito ambako atautazama mradi huo wa reli. Huku maofisa wa White House, wakisema kiongozi huyo atatangaza mambo mapya kuhusiana na afya, kilimo biashara na usalama.

Aidha, ilielezwa kuwa ziara hiyo iliahirishwa hadi mwaka 2024 na ikachelewweshwa zaidi kwa sababu ya Kimbunga Milton, jambo lililotilia mkazo kauli ya baadhi ya Waafrika kwamba bara lao bado halipewi kipaumbele na Marekani.

Ilielezwa kuwa Rais wa mwisho wa Marekani kufanya ziara katika mataifa ya kusini mwa Jangwa la Sahara alikuwa Barack Obama mwaka 2015. Mwaka 2022, Biden alihudhuria mkutano wa kilele wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu mazingira nchini Misri, kaskazini mwa Afrika.

Madini ndilo eneo muhimu ambalo Marekani na China wanashindania na China tayari imeshikilia madini muhimu ya bara la Afrika.

Ilielezwa kuwa kwa miaka, Marekani imekuwa ikijenga mahusiano barani Afrika kupitia biashara, usalama na misaada ya kiutu. Ila sasa hiyo reli ya kilomita 1,300 ni mkakati mpya na kwa kiasi fulani inawiana na ule mkakati wa China wa barabara na miundombinu barani Afrika.

Vile vile, ilielezwa kuwa kuendelea kustawi kwa mradi huo wa Marekani wa Lobito unategemea rais anayeingia madarakani Trump na mahusiano yake na bara la Afrika.

Maofisa wa serikali ya Marekani walisema nchi hiyo imedhamiria kutoa dola bilioni tatu kwa mradi huo wa Lobito Corridor na miradi mingine inayohusiana. Ikielezwa kuwa ufadhili zaidi umetoka kwa Umoja wa Ulaya, mataifa saba yaliyostawi kiviwanda duniani G7, muungano wa makampuni ya kibinafsi unaoongozwa na mataifa ya Magharibi pamoja na benki za Afrika.

Wengi wanaamini kwamba mradi huo wa Lobito ambao Biden ataondoka ofisini kabla kukamilika kwake, utaungwa mkono pia na Trump, kwakuwa miongoni mwa mambo anayoyapa kipaumbele rais huyo mteule, ni kuupunguza ushawishi wa China.

**AP/DW**

## Coastal Union yawaza 4-bora

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya juzi kufanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, wachezaji wa Coastal Union wamepania kumaliza ligi kwenye nafasi nne za juu.

Bao la dakika za nyongeza lililofungwa na Maulid Shaaban liliihakikishia Coastal Union pointi tatu muhimu ambazo zimewapaisha mpaka nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Mfungaji wa bao hilo, Shaaban, akizungumza na Nipashe jana kutoka Arusha, alisema ushindi huo ni muhimu sana kwapo katika kukoleza nia yao ya kutaka kumalizi ligi kwenye nafasi nne za juu.

"Nimefurahi sana kuiwezesha timu yangu kupata ushindi, kama wachezaji tunatamani sana kumaliza katika nafasi za juu na ndio lengo letu kuwamo kwenye 'Top 4'," alisema Shaabn.

Mchezaji huyo alisema kila siku zinavyozidi kwenda ligi imekuwa ngumu, lakini wataendelea kupambana kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michezo yao.

"Kama wachezaji tunahitaji kujituma sana, Ligi imekuwa ngumu na tunaelekea kumaliza mzunguko wa kwanza, tutapambana katika kila mchezo kwa sababu tunatamani sana kumaliza kwenye nafasi nne za juu," alisema Shaaban.

## Uhamiaji yataka kumaliza na sita

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

PAMOJA na Uhamiji FC kuvuna alama tatu za kwanza baada ya kushindwa kufanya hivyo katika michezo mitatu mfululizo iliyopita, imesema sasa inahitaji kuzoa pointi zote sita katika mechi zake mbili zilizosalia kukamilisha mzunguko huu wa kwanza.

Katika mchezo wake wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya New City uliopigwa Uwanja wa Mau A juzi, Uhamiaji FC iliibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msadizi wa timu hiyo, Abdulsalehe Abdallah, alisema licha ya kupata ushindi huo, alikiri kuwa ulikuwa mchezo mgumu.

Alisema wapinzani wao ni miongoni mwa timu ambazo hazipo katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo, hivyo nao walikuwa wakihitaji kupata ushindi mpango ambao unafanana na wao.

Alisema licha ya kushinda mchezo huo kwao, bado wanahitaji kubeba pointi zote sita katika michezo miwili iliyopo mbele yao ili kuona wanatoka nafasi waliyopo sasa.

"Bado kuna ukaribu mkubwa wa alama, ndio maana ukipoteza mechi moja unajikuta upo chini na ukishinda michezo michache unajikuta upo juu ya msimamo wa Ligi Kuu, bado tunahitaji kupata alama sita katika michezo yetu hii miwili," alisema.

# KOCHA PRISONS ALIA MWAMUZI KUWATOA MCHEZONI WACHEZAJI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Mbwana Makata, amesema mwamuzi wa mchezo kati ya timu yake hiyo na Coastal Union, uliochezwa juzi katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, alifanya maamuzi mengi ambayo yaliwatoa wachezaji wake mchezoni kiasi cha kupoteza kwa mabao 2-1.

Akizungumza baada ya mchezo huo kumalizika, Makata alisema maamuzi aliyokuwa akifanya, yalikuwa yakiwakera, kuwakasirisha na kuwakatisha tamaa wachezaji wake na kwa kiasi kikubwa yalisababisha kuwatoa mchezoni na kucheza chini ya kiwango kipindi cha kwanza.

„Sitaki kumzungumzia sana mwamuzi, lakini kuna vitu alikuwa anavifanya akatutoa mchezoni, baadaye mapumziko niliwaambia vijana wangu wasihuzunike, badala yake warejee mchezoni, unaona kipindi cha pili tukarudi kwa nguvu na kusawazisha bao, tukakosa nafasi kadhaa za kufunga.

Baadaye Coastal wakabadilika wakaja na mipira mirefu, ilibidi nimtoe kiungo mmoja na kumuingiza beki mwingine wa kati kwenda kusaidia kuokoa kwa kupiga vichwa mpira ya juu, mwishoni tulizubaa wakatufunga bao la pili," alisema Makata.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mwambusi, alisema mpango alioingia nao kwenye mchezo huo kwa kujaza viungo wengi kati umemlipa.

"Katika mpango tuliokuja nao leo tuliweka viungo wengi ili waweze kuwachezesha mastraika mbele na watengeneze nafasi ambazo itawarahisishia kufunga mabao, na kwa kiasi kikubwa imetusaidia kuibuka na ushindi," alisema.

Mabao ya washindi kwenye mchezo huo yalifungwa na Hernest Malonga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 42, Maulid Juma alitupia sekunde chache kabla ya mechi kumalizika, Meschak Abraham akifunga bao la kufutia machozi kwa upande wa Prisons.

Matokeo hayo yanaipandisha Coastal hadi nafasi ya tisa ya msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 16, ikicheza michezo 13, huku Prisons ikisalia nafasi ya 13, ikiwa na pointi 10 kwa michezo 12 iliyocheza mpaka sasa.

**MAHAFALI...**



Brasi Bendi ya Jeshi la Wananchi (JWTZ), ikitumbuiza katika Mahafali ya 19 ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rombo Marathon Festival zaiva

**Na Grace Mwakalinga**

WANARIADHA na wadau wa michezo kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi, wanatarajiwa kushiriki mbio za Rombo Marathon Festival, zitakazofanyika Desemba 23, mwaka huu, katika viwanja vya Kilombero vilivyopo Longai wilayani Rombo, Kilimanjaro.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya Rombo Marathon Festival, Prof. Adolph Mkenda, Mbunge wa Jimbo la Rombo, ambaye pia ni Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, alisema ni msimu wa tatu, mbio hizo zinafanyika.

Alisema mbio hizo zitawahusisha wanariadha maarufu na wananchi wanaopenda michezo kama sehemu yao ya kujenga afya na kufurahi pamoja.

"Ni duru ya tatu sasa tunafanya hii Rombo Marathon Festival, ambazo zitakuwa na shughuli mbalimbali kama vyakula vya kienyeji, ndafu choma, kwa hiyo licha ya kuwa washiriki watafanya riadha, lakini pia watakula na kunywa, nawahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika mbio hizi ambazo zitafika hadi kilomita 10, kutakuwa na fursa watu kujionea uzuri wa misitu yetu ya asili ,"alisema Prof. Mkenda.

Aliongeza kuwa, marathon hiyo imekuwa na mchango mkubwa, katika kuinua vipaji vya wananchi wa Rombo na kutoa fursa kufanyika michezo mingine kama mashindano ya mpira wa miguu kupitia Mkenda Cup.

Alisema kufanyika kwa michezo na mashindano hayo kumeleta tija kwa sababu fedha zinazopatikana kupitia shughuli hizo, zimesaidia kujenga vyoo kwenye shule mbalimbali za serikali na kuboresha miundombinu ya Hospitali ya Huruma iliyopo wilayani humo.

Alisema wataendelea kuandaa na kufanya mashindano hayo ili kupata fedha zitakazosaidia kuboresha miundombinu ya afya na elimu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DALOT ATAKIWA MADRID

REAL Madrid imewasiliana na beki wa Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 25, na wameambiwa Manchester United inataka pauni milioni 41.5. Hata hivyo, beki wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26, atabakia kuwa kipaumbele cha mabingwa hao wa Hispania. ***(Relevo)***

### SALAH NA MKATABA

WINGA wa Misri, Mohamed Salah, yuko tayari kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja katika Klabu ya Liverpool, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, anazidi kukasirishwa na jinsi klabu hiyo inavyoshughulikia mazungumzo. (***Athletic)***

### PSG BADO KWA MO

KLABU ya Paris St-Germain haijafanya mazungumzo na Mohamed Salah licha ya kuhusishwa na winga huyo. ***(Sky Sports)***

### CONCEICAO AWANIWA

KLABU ya West Ham inamfikiria Kocha wa Porto, Sergio Conceicao, kuchukua nafasi ya Julen Lopetegui, ambaye mustakabali wake kama kocha unakabiliwa na shinikizo kubwa. ***(Guardian)***

### DIALLO KUONGEZEWA

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, anatazamiwa kufanya mazungumzo kuhusu mkataba mpya na winga wa Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 22, ambaye mkataba wake unakamilika msimu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### SANE MKATABA MPYA

KLABU ya Bayern Munich imeanza mazungumzo ya kuongeza mkataba wa winga wa Ujerumani, Leroy Sane, 28. ***(Sky Germany)***

### EDOUARD KUSITISHWA

KLABU ya Leicester City inafikiria kusitisha mkataba wa mkopo wa msimu mzima wa mshambuliaji wa Crystal Palace, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 26, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

### ROONEY HALI NGUMU

WAYNE Rooney anapigania kibarua chake kama Kocha wa Plymouth Argyle baada ya matokeo mabaya. Mechi zijazo za nyumbani dhidi ya Oxford United na Swansea City zinakadiriwa kuwa muhimu. ***(Telegraph)***

### ASENCIO KUONGEZEWA

REAL Madrid wanapanga kumpa beki wa Hispania, Raul Asencio, mkataba mpya wenye masharti bora zaidi. ***(Fabrizio Romano)***

### VILLA YATAKA BEKI

KLABU ya Aston Villa italenga beki mpya wa kulia kwenye dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***


### EDERSON AGOMBEWA

KLABU za Manchester United, Manchester City na Liverpool zote zinamtaka kiungo wa kati wa Atalanta na Brazil, Ederson, lakini itahitaji ofa kubwa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(TeamTalks)***

### KIWIOR KUONDOKA ARSENAL

FIORENTINA na Napoli zinatazamia mkataba wa mkopo kwa mlinzi wa Arsenal, Jakub Kiwior lakini kuna uwezekano kocha Mikel Arteta atamruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 24 kuondoka Januari. ***(Tuttomercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JORGINHO: ARSENAL BADO INA NAFASI EPL

●●●Tunahitaji kujaribu na kutumia nguvu zetu tukiwa nyumbani kushinda kadri tuwezavyo...

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Jorginho, amedai kwamba mwenendo mzuri wa timu yake kwenye mechi za nyumbani katika kipindi hiki cha kuelekea Sikukuu ya Krismasi unaweza kuwasaidia katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu ya England dhidi ya Liverpool.

'Washikabunduki' hao waliwafunga West Ham United mabao 5-2 Jumamosi na kukaa nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Bado kuna mechi 25 za Ligi Kuu na pointi 75 zinapatikana, lakini uamuzi wa taji la kila timu utajaribiwa katika mwezi ujao.

Arsenal na Liverpool zote zina mechi tisa kabla ya mapumziko mafupi ya wiki na nusu katika ratiba ya Ligi Kuu kwa mechi tatu za Kombe la FA.

Kikosi hicho cha kocha Mikel Arteta kinatazamiwa kucheza mechi nne za nyumbani katika michezo mitano ijayo, kuanzia na ziara ya leo Jumatano dhidi ya Manchester United.

Kwa kulinganisha, ni mechi moja tu kati ya sita zinazofuata za Liverpool itakayofanyika Anfield dhidi ya Fulham Desemba 14.

Jorginho aliwaambia waandishi wa habari: „Nadhani inaweza kusaidia. Lakini tunahitaji kuwa tayari kwa lolote na kujaribu kushinda katika mazingira yoyote. Tunahitaji kujaribu na kutumia nguvu zetu tukiwa nyumbani kushinda kadri tuwezavyo."

Arsenal ni moja kati ya klabu tatu za Ligi Kuu England ambazo bado hazijapoteza nyumbani msimu huu.

# Fernandes azua hofu Man United

**MANCHESTER, England**

NAHODHA wa Manchester United, Bruno Fernandes, alionekana akiwa na kifurushi cha barafu kwenye kifundo cha mguu baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Everton Jumapili, na hivyo kuzua hofu kwamba huenda akakosa mechi dhidi ya Arsenal leo Jumatano.



Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alitoa pasi za mabao mawili ya kwanza kwa 'Mashetani Wekundu' hao dhidi ya 'The Toffees', huku Marcus Rashford na Joshua Zirkzee kila mmoja akifunga mara mbili na kocha Ruben Amorim akipata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu England.

Hata hivyo, kocha mkuu mpya ameshtushwa na taarifa kuhusu jeraha kwa Fernandes, ambaye alichechemea muda mfupi baada ya filimbi ya mwisho.

Fernandes ana rekodi nzuri linapokuja suala la kuzuia majeraha, baada ya kulazimishwa tu kukosa mechi tatu za United tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2020.

Pia amekuwa na kiwango chake bora tangu Erik ten Hag atimuliwe kama kocha baada ya mwanzo mgumu, nyota huyo wa zamani wa Sporting CP ana mabao matano na asisti nne katika mechi nane za mwisho alizocheza kwa klabu na nchi.

Amorim tayari amekiri Fernandes atakuwa na jukumu kubwa katika kipindi chake ndani ya Old Trafford, akidokeza kuwa anaweza kucheza katika nafasi ya kiungo cha ndani zaidi siku zijazo.

Hata hivyo, alicheza nyuma ya Zirkzee pamoja na Rashford Jumapili, huku Mainoo na Casemiro wakifanya kazi katikati ya uwanja.

# Nisterlooy kuibakisha Leicester EPL

**LONDON, England**

KOCHA Ruud van Nistelrooy analenga kuleta hisia chanya kwa Leicester City na kuwavutia haraka wachezaji wa klabu hiyo, huku akiangalia kuhakikisha kwamba wanabakia kwenye Ligi Kuu England.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United aliteuliwa Ijumaa kuchukua nafasi ya Steve Cooper, huku klabu hiyo iliyo nafasi ya 16 ikielea juu ya eneo la kushushwa daraja baada ya kupoteza mara tatu mfululizo kwenye ligi.

Van Nistelrooy alitazama akiwa jukwaani Jumamosi Leicester ilipochapwa mabao 4-1 na Brentford huku kuajiriwa kwake kutomruhusu muda wa kutosha kuchukua jukumu la mchezo huo kwenye Uwanja wa Gtech Community.

Alipoulizwa ikiwa wachezaji wanahitaji kuboresha viwango vyao, Van Nistelrooy aliwaambia waandishi wa habari Jumatatu: "Hilo ndilo lililohitajika kufanywa. Jumapili ilikuwa mara ya kwanza kuwa hapa.

"Nilikuwa na mkutano na wachezaji na lilikuwa jambo la kwanza kushughulikia," alisema Mholanzi huyo.

"Hali tuliyomo, changamoto tunayokabiliana nayo, na kile kinachohitajika ili kutoka katika hali hiyo.


"Ndani ya siku mbili ni vigumu kufanya mabadiliko mengi, lakini tumeanza kufanya mabadiliko ya aina ya uchezaji, vipindi vya mazoezi, muundo, kidogo kidogo tunaanza kujenga msingi wa timu yenye ari ya kutosha kuweza kushiriki ligi hii."

Leicester wana kibarua kigumu cha mechi zijazo Desemba hii ikijumuishwa mechi dhidi ya Brighton & Hove Albion, Newcastle United, Liverpool na Manchester City.

Leicester walifurahia taji la Ligi Kuu England mwaka 2016 chini ya kocha wa wakati huo Claudio Ranieri, lakini wakashushwa daraja mwaka 2023 kabla ya kurejea chini ya Enzo Maresca, ambaye kwa sasa anainoa Chelsea.

Van Nistelrooy alisema Maresca, ambaye alicheza naye Malaga, alikuwa na mchango mkubwa kwake kuchukua kibarua cha Leicester.

"Una nia ya kujua kuhusu watu wanaofanya kazi huko na Enzo, kuwa rafiki mkubwa na mwenza wa zamani wa timu, alikuwa wa kwanza kupiga simu," alisema Van Nistelrooy.



# RAIS WA PSG AMTAKA MO SALAH

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Paris Saint-Germain, Nasser Al Khelaifi, amekuwa akiwasiliana mara kwa mara na wakala wa Mohamed Salah, Ramy Abbas, kuhusu mustakabali wa winga huyo wa Misri, kwa mujibu wa ESPN.

Salah mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake na Liverpool unamalizika msimu huu wa majira ya joto na hivi karibuni amesema bado hajapokea ofa rasmi ya mkataba kutoka kwa klabu hiyo.

Salah amefurahia kampeni ya kuvutia akiwa amefunga mabao 13 katika mashindano yote msimu huu.

Liverpool waliwazidi kiwango mahasimu wao Manchester City katika ushindi wa mabao 2-0 Jumapili huku Salah akifunga bao la pili kwa mkwaju wa penalti dakika ya 78.

Ushindi huo umeipa Liverpool uongozi wa pointi tisa kileleni mwa Ligi Kuu England.

Baada ya ushindi huo, Salah alizungumza kuhusu kutokuwa na uhakika wa mustakabali wake kwa mara ya pili ndani ya siku nane.

"Kusema kweli iko kichwani mwangu," alisema akiiambia Sky Sports.

"Hadi sasa huu ni mchezo wangu wa mwisho kucheza dhidi ya City, kwa hiyo nilikuwa naenda kufurahia. Hali ilikuwa ya ajabu hivyo nitafurahia kila sekunde hapa. Natumaini tutashinda ligi tu na tutaona kitakachotokea."

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba kipaumbele cha Salah ni kubakia Liverpool, ambapo aliwasili kutoka AS Roma mwaka 2017.

Lakini kukosekana kwa mkataba mpya mezani hadi sasa, inamaanisha kambi yake imewasiliana na klabu nyingine.

PSG wamekuwa wakimwania Salah kwa muda mrefu na walijaribu kumsajili mara kadhaa hapo awali bila mafanikio.

HABARI MICHEZO

# MAFUNZO MZUKA JUU IKIIVAA CHIPUKIZI LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA timu ya Mafunzo FC kupoteza mchezo wao wa raundi ya 13 wakiwa ugenini, Kisiwani Pemba, imesema bado wachezaji wao wana ari kubwa ya kufanya vizuri katika mechi yao ya leo dhidi ya Chipukizi FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Abdalla Bakari, alisema kikosi chake kipo imara kuwavaa wapinzani wao hao ili kuhakikisha wanapata alama zakuwarejesha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema wanashuka uwanjani kucheza kwa tahadhari kubwa kwa kuwa wanawafahamu vizuri wapinzani wao hao hasa wakiwa katika dimba la nyumbani.

Bakari alisema katika uwanja wao wa mazoezi, wametumia muda mwingi kutoa darasa la la umakini jambo litakalowafanya kushindwa kutimiza lengo lao.

Alisema wamewaambia wachezaji wao kucheza kwa kutulia na kuwa makini wakati wanapomiliki mpira na hata wapopoteza mpira.

Kocha huyo aliweka wazi kuwa iwapo wachezaji watafuata maelekezo yote ya benchi la ufundi, wana uhakika wa kupata ushindi katika mchezo huo.

"Michezo yote ya ugeni ni migumu, kutokana na kila mmoja anataka kutamba katika uwanja wake wa nyumbani, hivyo tumejipanga kukabiliana na kila hali ili kuona mchezo huu wa 14 tunarudi na alama zote nyumbani," alisema.

Mafunzo FC itashuka dimbani leo ikiwa nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kujikusanyia pointi 26 kwa mechi 13, wakati kinara wa ligi hiyo ni Malndege FC ikiwa na alama 27.

# Feitoto aitamani michuano kimataifa

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Klabu ya Azam na Timu ya Taifa 'Taifa Stars' Feisal Salum 'Feitoto', amesema anatamani kuona timu hiyo ingeendelea kuwa kwenye michuano ya kimataifa, lakini bahati mbaya waliondolewa mapema.

Kiungo huyo amesema michuano hiyo ya CAF ndio inawafanya kwa sasa kupambana kwenye michezo ya Ligi Kuu ili kusaka tiketi ya kushiriki mashindano kimataifa mwakani.

Azam ilitolewa hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na APR ya Rwanda na kufuta ndoto zao za kufanya vizuri kwenye michuano hiyo msimu huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Feitoto alisema kila mchezaji anatamani kushiriki michuano hiyo ya kimataifa na wao kama Azam wanapambana kurejea tena msimu ujao.

"Kwa sasa nguvu zetu kama wachezaji tumezielekeza kwenye michezo yetu ya Ligi Kuu, tunataka kurejea kwa kishindo kwenye michuano ya CAF na tunafahamu mpaka tufanye vizuri kwenye ligi yetu," alisema Feitoto.

Alisema msimu huu kwenye michuano ya kimataifa hawakuwa na bahati na kujikuta wakitolewa mapema, lakini watarejea kwenye michuano hiyo kwa kishindo.

Azam imekuwa kwenye kiwango kizuri ambapo kwa sasa inaongoza kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 30 baada ya kucheza michezo 13, Simba inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 28, lakini ina michezo miwili pungufu sawa na Yanga inayoshika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 27.

MCHANGANI...



Wachezaji wa timu ya Kitunda ya jijini Dar es Salaam, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yatambia uzoefu mechi CAF

INATOKA UK. 24

ezo rahisi, utakuwa mgumu, kumbuka tutakuwa ugenini na timu za Afrika Kaskazini unazijua jinsi zilivyo ndani na nje ya uwanja, uzuri ni kwamba Simba tumekuwa wazoefu kwa mechi za aina hii," alisema.

Beki huyo wa kushoto, alisema mechi hiyo itakuwa ni ya kimbinu zaidi, huku akisema kwa kiasi kikubwa watakuwa wanamsikiliza kocha wao, Fadlu Davids atakapokuwa anawaelekeza cha kufanya wakati mchezo ukiendelea.

"Najua wao wana video zetu watakuwa wanatuangalia, lakini sisi pia tunazo kila mmoja kaangalia ubora na madhaifu ya mwenzake, lakini wakati mechi inaendelea mifumo na plani zinabadilika kutokana na mpinzani anafanya nini, bahati nzuri tuna mwalimu mzuri sana na benchi la ufundi watatuelekeza ni jinsi gani ya kuicheza mechi hiyo hatua kwa hatua mechi itakapokuwa inaendelea, naamini tunakwenda kufanya vizuri na mechi hii itaamua nani atakaa kileleni, nani ataongoza kundi, na sisi nia yetu ni kuongoza kundi tulilopo," alisema.

Simba ipo Kundi A, ikiwa pamoja na timu za Bravo do Maquis ya Angola, CS Contantine ya Algeria na CS Sfaxien ya Tunisia.

Simba na CS Contantine kila moja ina pointi tatu na bao moja baada ya kushinda kwenye mechi yao ya kwanza.

Kila timu ilipata ushindi wa bao 1-0, Simba ikiifunga Bravo do Maquis nyumbani, CS Contantine, ikipata ushindi kama huo pia ugenini nchini Tunisia.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed amesema kikosi hicho kiliondoka na ndege kuelekea nchini Uturuki, ambapo kitachukua ndege ya pili itakayowafikisha mji mkuu wa Algeria, jijini Algiers, ambako nako watatwaa ndege nyingine ya tatu kuelekea kwenye mji wa Constantine.

"Tukifika Uturuki, tutachukua ndege nyingine mpaka Algeria jijini Algiers, tukitoka hapo tutakwenda mjini Constantine ambapo ni mwenzo wa saa tano mpaka sita kwa mwendo wa basi na saa moja mpaka dakika 55 kwa usafiri wa ndege ambao ndiyo tutakaoutumia hadi huko.

"Taarifa tulizozipata kuna baridi kali sana, lakini tunakwenda kupambana tukiwa na malengo mawili ambayo tumeyaweka, nayo ni kushinda mchezo huo na kama ikiwa ngumu sana basi tutoke hata sare," alisema Ahmed.

# Michezo


Jumatano Desemba 4, 2024
Nipashe

## Jorginho: Arsenal bado ina nafasi EPL

UKURASA 21



TUPO TAYARI...




Wachezaji wa Timu ya Yanga wakiwa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana alasiri, tayari kwa safari ya kuelekea Algeria kwa mechi yao ya Kundi A, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger itakayopigwa Jumamosi saa nne usiku kwa saa za Afrika Mashariki. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA YATAMBIA UZOEFU MECHI CAF

●●●Wachezaji wasifu mbinu za Kocha Fadlu, wasema wanataka kukaa kileleni, watumia ndege tatu hadi...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji 22 wa Simba, benchi la ufundi na viongozi kadhaa kimeondoka alfajiri ya leo kwenda nchini Algeria kwa ajili ya mchezo wa pili, Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi dhidi ya CS Constantine, huku nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein ,Tshabalala, akisema wanakwenda kusaka ushindi ili wawe vinara wa Kundi A.

Kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, kikosi hicho kitatumia ndege tatu mpaka kufika mjini Constantine utakapopigwa mchezo huo, Jumapili Ijayo, Uwanja wa Mohamed Hamlaoui, saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Nahodha wa timu hiyo, Tshabalala amesema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wanakwenda kukamilisha kile ambacho wamekifanya kwenye uwanja wa mazoezi.

"Yalikuwa maandalizi mazuri sana, niseme tu tumejiandaa vizuri ili kwenda kupambana, hautakuwa mch-

INAENDELEA UK. 23

## Ramovic: Hatutakubali fedheha kwa MC Alger

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kabla ya mchezo wao wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger, Kocha wa Yanga, Saed Ramovic, amesema watachukua tahadhari kwenye mechi hiyo kwani itakuwa fedheha kama watapoteza michezo miwili mfululizo katika kundi lao.

Yanga jana ilisafiri kwenda Algeria kwa ajili ya mchezo huo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi utakaopigwa Jumamosi saa nne usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kuanza safari jana, Ramovic alisema wamejiandaa vizuri na hawataki kuweka kumbukumbu ya mchezo wao wa kwanza dhidi ya Al Hilal ambao walipoteza nyumbani kwa mabao 2-0.

„Hatua hii kila mchezo ni mgumu, tunaenda kucheza na timu nzuri kama zilivyo nyingine, tutakuwa makini kwa muda wote tukiwa na lengo la kupata ushindi, wachezaji wangu wanafahamu umuhimu wa mchezo huu hasa kutokana na kupoteza wa kwanza," alisema Ramovic.

Alisema kupoteza mchezo wao wa kwanza imekuwa funzo kwao kuelekea kwenye michezo iliyobaki katika kundi lao.

"Hatupo tayari kupoteza mchezo wa pili mfululizo, ni lazima tupambane kupata ushindi ili kuwa kwenye nafasi nzuri, naamini tunaweza kufanya vizuri kutokana na maandalizi yetu kuelekea kwenye mchezo huu," alisema.

Nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, alisema mchezo huo wa pili ni muhimu sana katika harakati za kutaka kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

"Tunafahamu mashabiki wana imani kubwa na sisi wachezaji, tunaenda ugenini, lakini tunaenda kupambana, tunafahamu umuhimu wa mchezo huu," alisema Mwamnyeto.

Yanga itacheza mchezo huo wa pili hatua ya makundi ikiwa mkiani mwa Kundi lao la A, baada ya kupokea kipigo cha mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Al Hilal ya Sudan, huku wenyeji wao, MC Alger wakitoka kulazimisha suluhu ugenini dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika mechi yao ya kwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >